Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura yaTatu

## Wakati wa Kanisa la Efeso

### Utangulizi Wa Nyakati Za Kanisa

Ili mpate kufahamu kabisa ujumbe wa Nyakati za Kanisa ningetaka kuelezea kanuni mbalimbali zilizoniruhusu kuyapata majina ya wale wajumbe, urefu wa nyakati, na mambo mengine yanayohusika humo.

Kwa kuwa somo hili lilipaswa kuwa zito kuliko yote niliyopata kuchukua hadi wakati huu, nilimwomba Mungu kwa siku nyingi anipe upako wa Roho Mtakatifu. Na hapo tu ndipo niliposoma Maandiko juu ya Nyakati za Kanisa na kuchunguza kwa makini sana historia kadha wa kadha za kanisa zilizoandikwa na wanahistoria nilioweza kupata wasiopendelea kabisa upande wo wote. Mungu hakuacha kuyajibu maombi yangu, kwa maana wakati nilipokuwa nikisoma Neno na historia kadha wa kadha, niliwezeshwa na Roho Mtakatifu kuona utaratibu ukijifunua ambao ulidumu katika zile karne na hata kufikia moja kwa moja katika siku hii ya leo, ya mwisho.

Ufunguo niliopewa na Bwana ambao kwa huo niliweza kuamua mjumbe kwa kila wakati ni wa Kimaandiko kabisa. Kwa kweli huenda ukaitwa Jiwe la Msingi la Biblia. Ni ule ufunuo ya kwamba Mungu habadiliki hata kidogo, na ya kwamba njia Zake hazibadiliki kama jinsi tu Yeye asivyobadilika. Katika Ebr. 13:8 inasema

> *"Yesu Kristo yeye yule jana, na leo, na hata milele."*

Mhubiri 3:14,15,

> *"Najua ya kwamba, kila kazi aifanyayo Mungu, itadumu milele: haiwezekani kuizidisha kitu, wala kuipunguza kitu: nayo Mungu ameifanya, ili watu wamche Yeye.*
>
> *Yale yaliyoko yamekuwako; na hayo yatakayokuwako yamekwisha kuwako; na Mungu huyatafuta tena mambo yale yaliyopita."*

Hili hapa: Mungu asiyebadilika mwenye njia zisizobadilika. Yale aliyofanya mara ya KWANZA Yeye hana budi kuendelea kuyafanya mpaka yatakapofanywa kwa mara ya MWISHO. Hakutakuwa na badiliko kamwe. Weka hilo kwenye Nyakati za Kanisa. Aina ya mtu ambaye Mungu alimchagua kwa wakati wa kwanza, na jinsi ambavyo Mungu alijidhihirisha katika huduma ya mtu huyo, itakuwa ndio mfano kwa ajili ya nyakati nyingine zote. Kile Mungu alichofanya katika wakati wa kwanza wa kanisa ndicho anachotaka kufanya katika nyakati zingine zote.

Sasa tunajua kabisa kutokana na Neno ambalo liliandikwa na Roho Mtakatifu jinsi kanisa la kwanza, la asili, lilivyoanzishwa na jinsi Mungu alivyojidhihirisha Mwenyewe ndani Yake. Neno haliwezi kubadilika wala kubadilishwa kwa sababu Neno ni Mungu. Yohana 1:1,

> *"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu."*

Kubadilisha Neno lake moja, kama alivyofanya Hawa, kunaleta dhambi na mauti, kama vile pia inenwavyo katika Ufu. 22: 18-19,

> *"... Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki:*
>
> *Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika kile Kitabu cha Uzima, na katika ule mji mtakatifu, na kutoka katika mambo yaliyoandikwa katika kitabu hiki."*

Hivyo basi, vile kanisa lilivyokuwa wakati wa Pentekoste ndicho kipimo. Hicho ndicho kielelezo. Hakuna kielelezo kingine. Haidhuru wasomi wanasema nini, Mungu HAJABADILISHA kielelezo hicho. Yale Mungu aliyofanya kwenye Pentekoste hana budi kuendelea kuyafanya mpaka nyakati za kanisa zitakapofungwa.

Ingawa wasomi wanaweza kukwambia wakati wa mitume umekwisha, usiamini jambo hilo. Tamshi hilo ni kosa kwa sababu mbili. Kwanza kabisa, ni makosa kudhani hakuna mitume wengine zaidi, kwa sababu tu wale kumi na wawili wa kwanzai wamekufa. Mtume maana yake ni 'yeye aliyetumwa'; na kuna wengi waliotumwa leo, lakini wanaitwa wamishenari. Mradi tu watu wanaitwa na kutumwa wakiwa na Neno la Uzima wakati wa mitume upo unaendelea. Pili, wao wanazungumzia siku za 'nguvu za Roho Mtakatifu

zilizodhihirishwa' kuwa kwamba zimekwisha kwa kuwa Biblia imekamilishwa. Hilo si kweli. Hakuna hata Andiko moja linalodokeza jambo hilo, lakini mengi yanasema vinginevyo. Hili hapa thibitisho letu ya kwamba mashtaka hayo mawili ni ya uongo. Matendo 2:38, 39.

> *"Basi Petro akawaambia, Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*
>
> *Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."*

Ahadi za nguvu ambazo mitume walipewa wakati wa Pentekoste ni "kwa ajili yenu (Wayahudi), na kwa watoto wenu (Wayahudi), na kwa watu wote walio mbali (Mataifa), na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie (Wayahudi na Mataifa pia)". Mpaka atakapoacha kuita, ujumbe wa Pentekoste na nguvu zake HAVITAKOMA.

Kile kanisa lilikuwa nacho kwenye Pentekoste ni haki yake isiyoweza kuondolewa. Mwanzoni, lilikuwa na Neno safi la Mungu. Lilikuwa na nguvu za Roho zilizodhihirishwa katika ishara na maajabu mbalimbali na karama za Roho Mtakatifu. Waebrania 2:1-4,

> *"Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa, tusije wakati wo wote tukayakosa.*
>
> *Kwa maana ikiwa lile Neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi (kwa Neno) ulipata ujira wa haki;*
>
> *Sisi je! tutapataje kupona, tusipojali waokovu mkuu namna hii; ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliomsikia Yeye;*
>
> *Mungu naye akishuhudia pamoja nao, kwa ishara na maajabu, na nguvu za namna nyingi, na vipawa vya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda Mwenyewe?"*

Hilo kanisa la asili halikuundwa na wanadamu. Iliongozwa na Roho Mtakatifu. Halikuwa kubwa sana. Ilichukiwa na kudharauliwa. Lilikandamizwa. Iliteswa hata kufa. Lakini lilikuwa aminifu kwa Mungu. Lilidumu na kile kielelezo cha asili cha Neno.

Sasa msipotoshwe hapa. Niliposema ya kwamba Mungu na njia Zake hazibadiliki, sikusema ya kwamba kanisa na wajumbe wake wasingeweza kubadilika. Kanisa si Mungu. Kwa hiyo linaweza kubadilika. Lakini nililosema ni kwamba kwa sababu ya Mungu asiyebadilika na njia zisizobadilika tunaweza tukarudi nyuma huko mwanzo na kuona tendo la kwanza na lililo kamilifu la Mungu halafu tuamue kwa kipimo hicho. Hivyo ndivyo inavyofanyika. Kanisa la Kweli daima litajaribu kuwa kama la asili huko Pentekoste. Kanisa la Kweli la siku hizi litajaribu kulingana na lile la kwanza la mwanzoni. Nao wajumbe kwa makanisa, wakiwa na Roho yule yule wa Mungu ndani yao, watajaribu kulingana na mtume Paulo. Hawatakuwa kama yeye kabisa; lakini wajumbe wa kweli watakuwa ni wale wanaomkaribia kabisa Paulo, aliyekuwa hakufungwa na mtu ye yote, aliyejitolea kabisa kwa Mungu, na kuhubiri Neno la Mungu peke yake tu, na kumdhihirisha Roho Mtakatifu katika nguvu. Hakuna mwingine angeweza kufanya hivyo. Huna budi kuanzia na lile la mwanzoni. Kama vile mbegu izaavyo kwa jinsi yake, Kanisa la Kweli daima litakuwa ni lile linalojaribu kufuata nyayo za waanzilishi wake wa Pentekoste na wajumbe wake watamfuata mtume Paulo, yule mjumbe wa kwanza wa wakati wa kwanza wa kanisa. Ni rahisi jinsi hiyo, na ni zuri namna hiyo.

Nikiwa na ufunguo huu, ulio rahisi sana, hata hivyo ulio mzuri sana, niliweza, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, kukisoma Kitabu cha Ufunuo na historia kadha wa kadha na kupata humo kila wakati, kumpata kila mjumbe, kupata muda uliodumu kila wakati, na kazi kila mmoja aliyotenda katika kusudi la Mungu tangu Pentekoste hata ukamilifu wa nyakati hizo.

Kwa sababu sasa unafahamu jinsi tunavyoamua Kanisa la Kweli lilivyokuwa (jinsi lilivyokuwa wakati wa Pentekoste na jinsi lilivyokuwa katika nyakati za mitume kama ilivyoandikwa katika Neno katika Kitabu cha Matendo) tunaweza kutumia kanuni ile ile kutuonyesha jinsi kanisa lilivyoshindwa. Kosa la msingi, ama makosa, yaliyopenyeza katika kanisa la kwanza na yakafunuliwa katika Kitabu cha Matendo na Ufunuo na pia katika zile Nyaraka yatazidi kudhihirishwa dhahiri zaidi na zaidi katika kila wakati unaofuata, mpaka tutakapofikia kuondolewa kabisa kwa ile kweli katika wakati wa mwisho, au Wakati wa Laodikia.

Sasa kutoka kwenye ufunguo huu wa kwanza ambao tumepokea kutoka kwa Bwana, kunakuja ukweli mwingine na wa ajabu kidogo. Nilisema ya kwamba Kanisa la Kweli daima litajaribu kuwa kama lilivyokuwa katika Kitabu cha Matendo. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini tumegundua ya kwamba Neno pia linafundisha kupenyeza kwa kosa mpaka kweli imeondolewa kabisa katika siku ya mwisho wakati Bwana yuko karibu kuonekana. Swali sasa linazuka mioyoni mwetu; je! Mungu huwaacha walio Wake na kuwaacha waingie katika hali ya udanganyifu kabisa? La hasha, kwa maana Maandiko yanasema dhahiri kabisa katika Mat.

24:24, ya kwamba 'Walio Wateule HAWAWEZI' kupotezwa.

> *"Kwa maana watatokea Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; kiasi kwamba wapate kuwapoteza KAMA YAMKINI, hata walio wateule."*

Itakuwaje basi? Jibu liko wazi mbele zetu. Kuna Kanisa la Kweli na kanisa la uongo. Kuna Mzabibu wa Kweli na mzabibu wa uongo. Lakini bila shaka kanisa hilo la uongo, kundi hilo la mzabibu wa uongo, daima litajaribu kunyakua mahali pa Kanisa la Kweli na kudai ya kwamba lenyewe, wala si walio Wateule, ndio walio halisi na wa kweli. La uongo litajaribu kuliua la Kweli. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika Kitabu cha Matendo, hivyo ndivyo ilivyofafanuliwa katika zile nyakati saba, na hivyo ndivyo ilivyonenwa kwa udhabiti katika Nyaraka mbalimbali. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Hivyo ndivyo ilivyo sasa. Hivyo ndivyo itakavyokuwa. Haiwezi kubadilika.

Sasa hebu na tuwe waangalifu sana ya kwamba hatuchanganyikiwi hapa. Kwa hivyo tutatafuta Neno kuthibitisha dai hili. Hebu na turudi kwenye Kitabu cha mwanzo, Mwanzo. Katika Bustani ya Edeni kulikuwako na miti MIWILI. Mmoja alikuwa mzuri; mmoja alikuwa mwovu. Mmoja ulizaa UZIMA, huo mwingine ulizaa Mauti. Kulikuwa na watoto wawili ambao ndio kwa mara ya kwanza kabisa walimtolea Mungu dhabihu. Hebu nirudie jambo hilo, WOTE WAWILI walimtolea Mungu dhabihu. Mwanzo 4:3-5,

> *"Ikawa hatimaye, Kaini akaleta mazao ya ardhi sadaka kwa Bwana.*
>
> *Habili naye, akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake:*
>
> *Bali Kaini hakumtakabali wala sadaka yake..."*

Lakini mmoja (Kaini) alikuwa mwovu, akiwa wa baba yake (yule Mwovu), wakati Habili alikuwa mwenye haki mbele za Bwana. Tena, kulikuwako na watoto wawili kutoka katika mwili wa wazazi wale wale. Walikuwa ni mapacha wa Isaka na Rebeka. Mmoja alikuwa ni mteule wa Mungu na mwingine alikuwa amekataliwa. Wote wawili walimwabudu Mungu. Katika kila kisa kimojawapo kulikuweko na kumwabudu Mungu. Katika kila kisa yule mwovu alimchukia mwenye haki na kumtesa mwenye haki. Wakati mwingine yule mwovu alimwangamiza mwenye haki. Lakini angalia. Walipandwa pamoja. Waliishi pamoja. Wote wawili walimwomba Mungu na kumwabudu Mungu.

Mifano hii inaonyesha kikamilifu mfano wa Bwana Yesu Kristo hapo aliposema ya kwamba ufalme wa mbinguni unafananishwa na mtu aliyepanda mbegu njema, lakini adui akaja akapanda magugu miongoni mwa mbegu hizo njema. Mungu hakupanda magugu. Shetani alipanda hayo magugu moja kwa moja miongoni mwa mbegu nzuri ya Mungu. Hizo aina mbili za mimea (watu), kutoka kwenye mbegu mbili mbalimbali, zilikua pamoja. Zilikula chakula katika udongo ule ule, zilishiriki jua lile lile, mvua, na baraka nyingine zote, na zote mbili zilivunwa kwa wakati wao. Mnaona jambo hilo? Usisahau kamwe kweli hizi tunapojifunza nyakati za kanisa na baadaye ile mihuri. Na zaidi ya yote, usisahau ya kwamba ni katika wakati huu wa mwisho wakati magugu yanapofungwa matita-matita yapate kuteketezwa, ambapo wataisonga ngano ambayo itawekwa ghalani na Bwana.

Ninataka kufuatilia jambo hili mpaka nilimalizie, kwa hiyo hebu na twende hatua moja mbele zaidi. Umewahi kusoma historia ya miamsho? Sasa uamsho unamaanisha tendo la Mungu katika nguvu. Na kila wakati Mungu anapotenda kazi, Shetani naye yuko hapo kutenda kazi pia. Haikosekani. Katika siku za ule uamsho mkuu wa Kiwelshi (na karibu watu wote hawajui jambo hili), hospitali za wenda wazimu zilijaa upesi, na kulikuweko na onyesho kubwa la nguvu za ibilisi kuwazuia watu wasimsikilize Mungu. Imeandikwa ya kwamba katika wakati wa Wesley watu wangefanya vitu vya ajabu ajabu sana ambavyo dhahiri vilikuwa ni vya Shetani akijaribu kudhihaki wema na nguvu za Mungu. Katika siku za Luther inasemwa ya kwamba muujiza wa huduma yake haukuwa katika ukweli kwamba yeye alifaulu kulipinga Kanisa Katoliki la Kiroma, lakini muujiza ulikuwa katika ukweli wa yeye kuweza, na aliweza, kusimama imara na mwenye akili timamu kati ya washupavu wa dini ambao mara nyingi walijazwa, na kuongozwa, na pepo wachafu. Na kama una habari na huduma hii ya siku ya mwisho, utakuwa umeona uvamizi ule ule wa roho wabaya na wa waovu. Haina budi kuwa hivyo. Sasa ninatumaini na kuamini wewe ni wa kiroho vya kutosha kupata jambo hilo, na kulitilia maanani.

Ili kutia tu muhuri jambo hili juu ya mizabibu ya Kweli na ya uongo ikichanganyikana na kuonyesha zile roho mbili ambazo zinatenda kazi sasa, hebu na tuangalie katika I Yohana 4:1-4, na Yuda 3,4,12.

> *"Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho kwamba zimetokana na Mungu: kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea duniani.*
>
> *Katika hili mwamjua Roho wa Mungu: Kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu:*
>
> *Na kila roho isiyokiri ya kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili haitokani na Mungu: Na hii ndiyo roho ya mpinga-Kristo, ambayo mmesikia kwamba ilipaswa kuja; na SASA*

*IMEKWISHA KUWAKO duniani.Na kila roho isiyokiri ya kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili si ya Mungu; na hii ni roho ya mpinga Kristo, ambayo mmesikia ya kwamba inakuja; na hata sasa ni tayari ulimwenguni.*

*Ninyi watoto wadogo, mwatokana na Mungu; nanyi mmewashinda: (roho ya mpingaKristo) kwa sababu Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, (Roho wa Mungu) kuliko yeye aliye katika dunia."*

Yuda 3,4,12.

*"Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliyokabidhiwa WATAKATIFU mara moja tu.*

*Kwa maana kuna WATU (si Watakatifu) waliojiingiza kwa siri (hawa hawakuingia katika kundi kwa kupitia MLANGONI na kwa hiyo wao ni wanyang'anyi), watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, MAKAFIRI, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana Yeye Aliye peke Yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo.*

*Watu hawa ni miamba yenye hatari katika karamu zenu za upendo, walapo karamu PAMOJA nanyi, wakijilisha pasipo hofu..."*

Haliwezi kukanushwa mbele ya Maandiko haya ya kwamba Kanisa la Kweli na kanisa la uongo yameshikamana, yakiwa yamepandwa pamoja lakini ni ya mbegu tofauti.

Sasa basi, nafikiri kuna jambo lingine mnalopaswa kujua. Makanisa hayo saba ambayo yanayoandikiwa na Yohana yapo Asia Ndogo na yote ni makanisa ya Mataifa.. Yeye hasemi na kanisa la Yerusalemu ambalo lilikuwa ni Wayahudi labda likiwa na Mataifa wachache tu ndani yake. Sababu ni kwamba Mungu alikuwa amewaacha Wayahudi akawageukia Mataifa. Kwa hiyo nyakati zote za kanisa ni Mungu akishughulika na Mataifa, na kumwita Bibi-arusi Mmataifa Kwake. Hilo linazifanya 'Nyakati za Kanisa' na 'Utimilifu wa Mataifa' jambo lile lile tu. Matendo 13:44-48,

*"Hata sabato ya pili watu wengi, karibu mji wote, wakakusanyika walisikie Neno la Mungu.*

*Bali Wayahudi walipowaona makutano, wakajaa wivu, wakayakanusha maneno yaliyonenwa na Paulo, wakibisha na kutukana.*

*Ndipo Paulo na Barnaba wakanena kwa ushujaa, wakasema, Ilikuwa lazima Neno la Mungu linenwe kwenu kwanza: lakini kwa kuwa mnalisukumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele, angalieni, twawageukia Mataifa.*

*Kwa sababu ndivyo tulivyoamriwa na Bwana, akisema, Nimekuweka uwe nuru ya Mataifa, upate kuwa wokovu hata mwisho wa dunia.*

*Mataifa waliposikia hayo, wakafurahi, wakalitukuza Neno la Bwana: Nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini."*

Warumi 11:1-8,

*"Basi, nauliza, Je! Mungu aliwasukumia mbali watu Wake? Hasha! Kwa kuwa mimi nami ni Mwisraeli, mmoja wa wazao wa Ibrahimu, mtu wa kabila ya Benyamini.*

*Mungu hakuwasukumia mbali watu Wake aliowajua tokea awali. Au hamjui yale yaliyonenwa na Maandiko juu ya Eliya? jinsi anavyowashitaki Waisraeli mbele za Mungu, akisema,*

*Bwana, wamewaua manabii Wako, wamezibomoa madhabahu Zako; nami nimesalia peke yangu, nao wananitafuta roho yangu. Lakini ile jawabu ya Mungu yamwambiaje? Nimejisazia watu elfu saba, wasiopiga goti mbele ya sanamu ya Baali.*

*Basi ni vivi hivi wakati huu wa sasa yako mabaki waliochaguliwa kwa neema.*

*Lakini ikiwa ni kwa neema, haiwi kwa matendo tena; au hapo neema isingekuwa neema. Lakini ikiwa ni kwa matendo, basi isingekuwa tena neema: au hapo matendo yasingekuwa matendo.*

*Imekuwaje basi? Kitu kile ambacho Israeli alikuwa akikitafuta hakukipata; lakini wale waliochaguliwa walikipata, na wengine walitiwa uzito*

*(Kama ilivyoandikwa, Mungu aliwapa roho ya usingizi, macho hata wasione, na masikio hata wasisikie;) hata siku hii ya leo."*

Warumi 11:25- 29,

*"Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msijue siri hii, ili msijione kuwa wenye akili, ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Israeli, mpaka Utimilifu wa Mataifa uwasili.*

*Hivyo Israeli wote wataokoka: kama ilivyoandikwa, Mwokozi atakuja kutoka Sayuni, atamtenga Yakobo na maasia yake;*

*Na hili ndilo agano Langu nao, nitakapowaondolea dhambi zao.*

*Basi kwa habari ya Injili, wamekuwa adui kwa ajili yenu: bali kwa habari ya kule kuchaguliwa, wamekuwa wapenzi kwa ajili ya baba zetu.*

*Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito Wake."*

Makanisa haya saba yaliyoko Asia Ndogo yalikuwa na tabia fulani ndani yao, katika siku hizo za kale, ambazo zilikuja kuwa tunda lililokomaa la nyakati za baadaye. Zile Mbegu zilizopandwa kule nyuma zilitokea baadaye katika mavuno yaliyokomaa, kama vile Yesu alivyosema,

*"Kwa kuwa kama wakitenda mambo haya katika mti mbichi, itakuwaje katika mkavu"? Luka 23:31.*

**Ujumbe Kwa Wakati Wa Kanisa la Efeso**

Ufunuo 2:1-7

*Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso andika; Haya ndiyo anenayo Yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono Wake wa kuume, Yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu;*

*Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya: tena umewajaribu wale wajiitao mitume, na sio, ukawaona kuwa waongo:*

*Tena ulikuwa na subira, na kuvumilia, na umetaabika kwa ajili ya Jina Langu, wala hukuchoka.*

*Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza.*

*Basi kumbuka ni wapi ulikoanguka, ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza; lakini usipofanya hivyo naja kwako upesi, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu.*

*Lakini unalo neno hili, kwamba wayachukia matendo ya Wanikolai, ambayo na mimi nayachukia.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa; Yeye ashindaye nitampa kula matunda ya Mti wa Uzima, ulio katika bustani ya Mungu.*

**MJUMBE**

Mjumbe (malaika) wa kanisa la Efeso alikuwa ni mtume Paulo. Kwamba yeye alikuwa mjumbe wa wakati wa kwanza wa wakati wa Mataifa haiwezi kukanushwa. Ingawa Petro alipewa mamlaka ya kuwafungulia Mataifa milango, Paulo ndiye aliyepewa kuwa mtume wao na nabii. Yeye alikuwa Nabii-Mjumbe kwa Mataifa. Kazi yake ya kinabii, ambayo kwayo alipokea ufunuo kamili wa Neno kwa ajili ya Mataifa, ilimthibitisha kama mjumbe wao wa kimitume. Jambo hili walilikubali wale mitume wengine kule Yerusalemu. Wagalatia 1:12-19,

*"Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu, wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.*

*Maana mmesikia habari za mwenendo wangu zamani katika dini ya Kiyahudi, kwamba naliliudhi kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu:*

*Nami naliendelea katika dini ya Kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika taifa langu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu.*

*Lakini ilipompendeza Mungu, aliyenitenga tangu tumboni mwa mama yangu, na akaniita kwa neema Yake,*

*Alipoona vema kumdhihirisha Mwanawe ndani yangu, ili niwahubiri Mataifa habari Zake; mara sikufanya shauri na watu wenye mwili na damu:*

*Wala sikupanda kwenda Yerusalemu kwa hao waliokuwa mitume kabla yangu; bali*

*nalikwenda zangu Arabuni, kisha nikarudi tena Dameski.*

*Kisha, baada ya miaka mitatu, nalipanda kwenda Yerusalemu ili nionane na Petro, nikakaa kwake siku kumi na tano.*

*Lakini sikumwona mtume mwingine, ila Yakobo ndugu yake Bwana."*

Wagalatia 2:2,

*"Nami nalikwenda kwa kuwa nalifunuliwa, nikawaeleza Injili ile niihubiriyo katika Mataifa, lakini kwa faragha kwa hao walio wenye sifa, isiwe labda napiga mbio bure, au nalipiga mbio bure."*

Wagalatia 2:6-9,

*"Lakini wale wenye sifa ya kuwa wana cheo, (walivyokuwa vyo vyote, ni mamoja kwangu: Mungu hapokei uso wa mwanadamu:) nasema, hao wenye sifa hawakuniongezea kitu:*

*Bali kinyume cha hayo, walipoona ya kuwa nimekabidhiwa Injili ya wasiotahiriwa, kama vile Petro ya waliotahiriwa:*

*(Maana Yeye aliyemwezesha Petro kuwa mtume wa waliotahiriwa, Ndiye aliyeniwezesha mimi kwenda kwa Mataifa:)*

*Tena walipokwisha kuijua ile neema niliyopewa, Yakobo, na Kefa, na Yohana, wenye sifa kuwa ni nguzo, walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika; ili sisi tuende kwa Mataifa, na wao waende kwa watu wa tohara."*

Warumi 11:13,

*"Lakini nasema na ninyi, mlio watu wa Mataifa. Basi, kwa kadiri nilivyo mtume wa watu wa Mataifa, naitukuza huduma iliyo yangu."*

Paulo alianzisha kanisa huko Efeso yapata katikati ya karne ya kwanza. Jambo hili linatuwezesha kuweka tarehe ya mwanzo wa Wakati wa Kanisa la Efeso; kama B.K. 53.

Mtindo wake wa kuhudumu uliweka kielelezo ambacho wajumbe wote wa baadaye watajaribu sana kuiga, na kwa kweli inaweka kielelezo cha kila mhudumu wa kweli wa Mungu, ingawa hatafikia kiwango hicho katika milki ya kinabii kama alivyofanya Paulo. Huduma ya Paulo ilikuwa na sifa tatu na ilikuwa kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa, Paulo alikuwa mwaminifu kabisa kwa Neno. Hakuliacha kamwe, hata imgharimu nini. Wagalatia 1:8-9,

*"Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.*

*Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe."*

Wagalatia 2:11,14,

*"Lakini Petro alipokuja Antiokia, nalishindana naye uso kwa uso, kwa sababu alistahili hukumu."*

*"Walakini, nilipoona ya kuwa njia yao haiendi sawasawa na ile kweli ya Injili, nalimwambia Petro mbele ya wote, Ikiwa wewe uliye Myahudi wafuata desturi za Mataifa, wala si za Wayahudi, kwa nini unawashurutisha Mataifa kufauata desturi za Wayahudi?"*

I Wakorintho 14:36-37,

*"Au je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? au kuwafikia ninyi peke yenu?*

*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*

Angalia ya kwamba Paulo alikuwa hana madhehebu, lakini aliongozwa na Roho, kama vile Mungu alivyomwongoza Musa kuwatoa Israeli kutoka Misri. Halmashauri ya Yerusalemu haikumtuma Paulo, wala haikuwa na nguvu zo zote wala mamlaka juu yake. Mungu, na Mungu pekee, ndiye aliyemtuma na kumwongoza. Paulo hakuwa wa wanadamu, bali wa Mungu. Wagalatia 1:1,

*"Paulo, mtume, (si mtume wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali na Yesu*

*Kristo, na Mungu Baba aliyemfufua kutoka kwa wafu:)"*

Wagalatia 2:3-5,

*"Lakini Tito, aliyekuwa pamoja nami, naye ni Myunani, alilazimishwa kutahiriwa:*

*Na hiyo ni kwa ajili ya ndugu za uongo walioingizwa kwa siri, ambao waliingia kwa siri ili kuupeleleza uhuru wetu tulio nao katika Kristo Yesu, ili watutie utumwani:*

*Ambao hata saa moja hatukujitia chini yao, ili kwamba kweli ya Injili ikae pamoja nanyi."*

Pili, huduma yake ilikuwa katika nguvu za Roho, kwa njia hiyo akidhihirisha Neno lililonenwa na lililoandikwa. I Wakorintho 2:1-5,

*"Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima.*

*Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, Naye amesulibiwa.*

*Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi.*

*Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu:*

*Ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu."*

Matendo 14:8-10,

*"Na huko Listra palikuwa na mtu mmoja, dhaifu wa miguu, kiwete tangu tumboni mwa mamaye, ambaye hakuwa ametembea kabisa:*

*Mtu huyo alimsikia Paulo alipokuwa akinena: ambaye akamkazia macho na kuona ya kuwa ana imani ya kuponywa,*

*Akasema kwa sauti kuu, simama kwa miguu yako sawasawa. Akasimama upesi akatembea."*

Matendo 20:9-12,

*"Kijana mmoja, jina lake Eutiko, alikuwa ameketi dirishani, akalemewa na usingizi sana; hata Paulo alipoendelea sana kuhubiri, akazidiwa na usingizi wake akaanguka toka orofa ya tatu; akainuliwa amekwisha kufa.*

*Paulo akashuka, akamwangukia, akamkumbatia, akasema, Msifanye ghasia, maana uzima wake ungalimo ndani yake.*

*Akapanda juu tena, akamega mkate, akala, akazidi kuongea nao hata alfajiri, ndipo akaenda zake.*

*Nao wakamleta huyo kijana akiwa hai, wakafarijika sana.*

Matendo 28:7-9,

*"Karibu na mahali pale palikuwa na mashamba ya mkuu wa kisiwa, jina lake Publio; mtu huyu akatukaribisha kwa moyo wa urafiki, akatufanya wageni wake kwa muda wa siku tatu.*

*Ikawa babaake Publio alikuwa hawezi homa na kuhara damu. Paulo akaingia kwake, akaomba, akaweka mikono yake juu yake, na kumpoza.*

*Yalipokwisha kutendeka hayo wengine waliokuwa na magonjwa katika kisiwa wakaja wakapozwa."*

II Wakorintho 12:12,

*"Kweli ishara za mtume zilitendwa katikati yenu katika saburi yote, kwa ishara; na maajabu; na miujiza."*

Tatu, alikuwa na tunda dhahiri la huduma aliyopewa na Mungu. II Wakorintho 12:11,

*"Nimekuwa mpumbavu katika kusifu, ninyi mmenilazimisha. Maana ilinipasa nisifiwe na ninyi; kwa sababu sikuwa duni ya mitume walio wakuu kwa lo lote, nijapokuwa si kitu."*

I Wakorintho 9:2,

*"Kwa maana Ikiwa mimi si mtume kwa wengine, lakini bila shaka ni mtume kwenu ninyi: kwa maana ninyi ndinyi muhuri ya utume wangu katika Bwana."*

II Wakorintho 11:2,

*"Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi."*

Paulo alikuwa ndiye njia ya kuleta kundi kubwa la kondoo wa Mataifa; yeye aliwalisha, na kuwashughulikia, mpaka wakazaa tunda la haki na wakawa tayari kumlaki Bwana kama sehemu ya Bibi-arusi wa Mataifa.

Kwenye wakati wa kutoa ule Ufunuo, kulingana na mapokeo, Paulo alikuwa amekufa tayari kama mfia imani, bali Yohana alikuwa akiendelea badala yake vile vile hasa Paulo alivyokuwa amefanya katika siku za huduma yake. Kifo cha Paulo, kabla ya ule Ufunuo kutolewa, hakifutilii mbali ukweli kwamba yeye alikuwa ndiye mjumbe wa Wakati wa Kanisa la Efeso, kwa kuwa mjumbe wa kila wakati, haidhuru ni katika wakati gani anatokea ama anaondoka, ndiye anayeushawishi wakati huo kuelekea kwa Mungu kwa huduma inayodhihirishwa na Neno. Paulo alikuwa mtu wa aina hiyo.

**MJI WA EFESO**

Mji wa Efeso ulikuwa mmoja wa miji mitatu mikubwa sana ya Asia. Mara nyingi uliitwa mji wa tatu wa imani ya Kikristo, Yerusalemu ukiwa wa kwanza, na Antiokia ya pili. Ulikuwa ni mji tajiri sana. Serikali ilikuwa ya Kirumi lakini lugha ilikuwa ni Kiyunani. Wanahistoria wanaamini ya kwamba Yohana, Mariamu, Petro, Andrea na Filipo wote walizikwa katika mji huu mzuri. Paulo, aliyeanzisha imani ya kweli katika mji huu, alikuwa mchungaji hapa kwa muda wa miaka mitatu tu; lakini wakati alipokuwa hayuko pamoja na kundi hilo alikuwa anawakumbuka daima, kwa maombi. Timotheo alikuwa askofu wake wa kwanza. I Timotheo 1:1-3,

*"Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na Bwana Yesu Kristo, Ambaye ndiye taraja letu;*

*Kwa Timotheo, mwanangu hasa katika imani. Neema na iwe kwako, na rehema, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.*

*Kama vile nilivyokusihi ukae Efeso, nilipokuwa nikisafiri kwenda Makedonia, ili uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine."*

Jina lenyewe, Efeso, lina maana mbili za ajabu, "Uliolenga", na "Uliolegea." Jitihada kuu za wakati huu uliokuwa umeanza kwa utimilifu wa Roho, "kilindi cha Mungu," ambapo walikuwa wakilenga kwenye wito mkuu wa Mungu, zilianza kutoa nafasi kwa hali kidogo ya kutokuwa waangalifu. Kumfuata Yesu Kristo kwa uvuguvugu kulianza kidogo kujidhihirisha kwenyewe kama dalili ya kwamba katika nyakati zijazo gari la kimwili linaloitwa kanisa lingezama kwenye uovu wa "kilindi cha Shetani." Ulikuwa umekwisha kulegea na ulikuwa ukikengeuka. Tayari wakati huo ulikuwa unarudi nyuma. Ulikuwa umeuacha upendo wake wa kwanza. Ile mbegu ndogo sana iliyopandwa katika wakati wa Efeso ingekua siku moja kuwa roho ya ukengeufu mpaka ndege wote wachafu wa angani wangejifanyia viota kwenye matawi yake. Mmea huo mdogo ungeonekana kwa huyo Hawa Mpya (lile Kanisa Jipya) kama usio na madhara kabisa kwa mawazo ya binadamu hivi kwamba angedanganywa tena na Shetani. Wakati wa Kanisa la Efeso ulikuwa umempa nafasi ya kupata mambo yaliyo mazuri sana ya Mungu, na kwa kitambo kidogo wakati huu ulishinda, na baadaye ukalegea, na katika wakati huo wa kutojihami Shetani akapanda mbegu ya maangamizi kabisa.

Dini yenyewe ya Efeso inaonyesha mfano mkamilifu wa wakati huu wa kwanza wa kanisa na inaweka mwelekeo wa nyakati zijazo. Kwanza kabisa, lile hekalu lililopambwa sana la Diana, lililochukua miaka mingi sana katika kulijenga, mlikuwemo katika nyua zake zilizowekwa wakfu sanamu ya Diana iliyochujuka sana na yenye sura mbaya sana ambayo mtu angeweza kuwazia. Alikuwa hafanani kabisa na sanamu nyingine zo zote zilizowekwa katika mahekalu mengine yaliyowekwa wakfu kwa ajili yake. Alikuwa tu ni sanamu ya kike isiyo na umbo ambayo hatimaye ilitumbukia kwenye gogo la mti ambamo alichongwa. Na mikono yake miwili ilitengenezwa kwa fito mbili za kawaida za chuma. Jinsi jambo hili linavyoonyesha kikamilifu roho ya mpinga-Kristo iliyoachiliwa katika wakati wa kwanza. Hiyo hapo imeachiliwa katikati ya watu, na hata hivyo haikuchukua umbo la kuwashtua watu. Hata hivyo mikono hiyo miwili ya fito za chuma ilionyesha ya kwamba kusudi lake lilikuwa ni kuvunja-vunja kazi ya Mungu wakati roho hiyo ilipofanya mashambulizi yake. Na hakuna mtu aliyekuwa ana habari naye ama na lile alilokuwa anafanya. Lakini siku moja wangeona, wakati akiwa na mikono hiyo ya chuma 'matendo' yake yalikuja kuwa ni 'fundisho', na fundisho lake likawa sheria ya dola.

Utaratibu wa ibada ya hekalu pia unadhihirisha mambo sana. Kulikuwako, kwanza kabisa, makuhani waliokuwa matowashi. Ukuhani huu isioweza kuzaa ulitangulia kuonyesha utasa wa watu ambao wangeliacha Neno, kwa maana watu wanaodai kumjua Mungu mbali na Neno hawana uhai kama vile towashi asivyoweza kuzaa. Pili, ndani ya hekalu mlikuwemo na makasisi wa kike bikira waliokuwa

wakishughulika na shughuli za kidini za hekalu. Hii ilionyesha siku ambayo ibada na desturi, kawaida za dini na matendo, yangechukua mahali pa Roho Mtakatifu na madhihirisho ya vipawa vya Roho hayangelijaza tena hekalu la Mungu. Juu ya hao wote alikuweko kuhani mkuu, mtu mwenye nguvu za kisiasa na ushawishi kwa watu, akionyesha yale yaliyokuwa yanaendelea, ingawa hayakudhihirika sana, hiyo ni kusema, kanisa punde si punde lingewekwa chini ya uongozi wa mwanadamu na mipango ya mwanadamu na tamaa zake za mambo makuu na "Roho Mtakatifu anasema hivi" halingekuwa tena jambo halisi lililo hai. Na chini ya hao wote kulikuwako na watumwa wa hekalu ambao hawakuwa na hiari ya uchaguzi ila kutii serikali ya kidini. Hili linaweza kumaanisha kitu gani ila kwamba siku ingekuja wakati makasisi wenye mamlaka, kwa njama za kisiasa, msaada wa serikali, na kubadilisha Neno na Roho kwa kutwaa kanuni za imani na mafundisho ya sharti, na uongozi wa kibinadamu, wangewatia wafuasi utumwani wakati viongozi walijifurahisha kwa anasa za mali waliyopata kwa njia zisizo halali na kufurahia anasa zao chafu, na watu maskini ambao ilipaswa watumikiwe kulingana na mapenzi ya Mungu, sasa wakawa watumishi.

**YESU, MJUMBE WAKE NA MAKANISA**

Ufunuo 2:1,

*"...Haya ndiyo anenayo Yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono Wake wa kuume, Yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu."*

Huyu Ndiye Ambaye imesemwa, 'Yesu yuyu Huyu ndiye Bwana na Kristo PIA.' Huyo hapo, Bwana Mungu Mmoja Mwenyezi na wa Pekee, na hakuna mwingine zaidi Yake. Huyo hapo, Mwokozi ("... wokovu ni wa Bwana", Yona 2:9) akienda katikati ya makanisa katika zile nyakati zote saba. Kile alichokuwa katika wakati wa kwanza ndicho alicho katika nyakati zote. Kwa kila mwaminio, Yeye ni Yesu Kristo yeye yule, jana, na leo, na hata milele. Yale aliyofanya mara moja Yeye angali anafanya, na ataendelea kufanya.

Sasa utaona ya kwamba Yesu anatembea peke yake katikati ya makanisa Yake. Hakuna mtu mwingine pamoja Naye. Wala kweli hapawezi kuwa, kwa sababu Yeye peke Yake ndiye aliyeliletea wokovu wake, na akiwa amelinunua kwa damu Yake mwenyewe linakuwa ni mali Yake. Yeye ndiye Bwana na Mwalimu wake. Kanisa humpa Yeye utukufu wote na utukufu huo Yeye hataushiriki na mtu mwingine. Hakuna papa aliyeko pamoja Naye. Hakuna askofu mkuu pamoja Naye. Mariamu, mama wa mwili Wake wa duniani, hayuko pamoja Naye. Yeye haneni na kumgeukia Baba fulani, kwa maana Yeye Ndiye Baba. Yeye hageuki na kutoa maagizo kwa Roho Mtakatifu fulani, kwa maana Yeye ndiye Mungu, Roho wa milele, na Uzima Wake ndio unaotiririka na kudundadunda kanisani ukilipa uzima, na bila ya Yeye hakungekuwa na uzima wo wote. Wokovu ni wa Bwana.

Hakuna mtu aliyekuwa pamoja Naye wakati alipoikanyaga ghadhabu ya hasira ya tanuru ya moto. Hakuwa ni mwingine, ila YEYE Ambaye alining'inia msalabani na kutoa damu Yake. Yeye Ndiye Mwanzilishi na Mwenye Kutimiza imani yetu. Yeye ni Alfa na Omega wa wokovu wetu. Tumeposwa Naye wala si mwingine. Sisi si wafuasi wa kanisa. Sisi ni mali Yake. Neno Lake ni sheria. Kanuni za imani, mafundisho ya sharti, sheria ndogo na katiba hazina nguvu kwetu. Naam, ni Yesu PEKE YAKE Ndiye anayetembea katikati ya makanisa. Ni Mungu ndani ya kanisa Lake, akipenda na kufanya mapenzi Yake mema. Kamwe usisahau hilo. Una uhusiano mmoja tu na Mungu na Mungu ana uhusiano mmoja tu na wewe—huo ni YESU, na YESU PEKEE.

Huyo hapo pamoja na zile nyota saba katika mkono Wake wa kuume. Mkono wa kulia au mkono unaonesha nguvu na mamlaka ya Mungu. Zaburi 44:3,

*"Maana si kwa upanga wao walivyoimiliki nchi, wala si mkono wao uliowaokoa: bali mkono Wako wa kuume, naam, mkono Wako, na nuru ya uso Wako, kwa kuwa uliwaridhia."*

Katika mkono huo wa kuume wa nguvu kuna nyota saba, ambazo, kulingana na Ufu. 1:20, ni wajumbe wa makanisa saba. Hii inaonyesha ya kwamba uweza na mamlaka yenyewe ya Mungu viko nyuma ya wajumbe Wake wa kila wakati. Wao wanatoka wakienda katika moto na mamlaka ya Roho Mtakatifu wakiwa na Neno. Wao ni nyota kwa sababu wanaakisi nuru. Nuru wanayoakisi ni nuru Yake. Hawana nuru yao wenyewe. Wao hawawashi moto wao wenyewe kusudi kwamba watu waweze kutembea katika nuru ya cheche zao. Isaya 50:11. Ni usiku, kwa maana wakati huo ndipo nyota zinapotokeza. Ni usiku wa weusi wa dhambi, kwa maana ya watu wote (yaani ulimwengu mzima), umetenda dhambi na daima unapungukiwa na utukufu wa Mungu. Warumi 3:23.

Wajumbe hawa saba wanamjulisha Mungu kwa watu. Yeye awapokeaye, ampokea Yeye aliyewatuma. Yohana 13:20. Wananena na kutenda kwa mamlaka Yake. Yeye husimama nyuma yao kwa nguvu zote za Uungu. Mathayo 28:18-20,

*"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa MAMLAKA YOTE mbinguni na duniani.*

*Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu:*

*Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi: na, tazama, MIMI NIPO PAMOJA NANYI SIKU ZOTE, hata ukamilifu wa dahari (utimilifu wa nyakati).*"

Kwa hiyo hao hapo, wamejaa Roho Mtakatifu na imani, wamepamba moto kwa moto wa Mungu, wakilishikilia Neno la kweli, naye Huyo hapo amesimama akiwaunga mkono. Na wazia jambo hilo, hakuna mwamini hata mmoja wa wakati wo wote anayepaswa kulia moyoni mwake, "Loo! laiti ningalikuwa kule nyuma katika wakati wa kwanza wakati mitume walipotumwa kwanza." HAKUNA haja ya kuangalia nyuma. ANGALIA JUU! Mtazame Yeye ambaye hata sasa anatembea katikati ya makanisa katika nyakati zote. Mtazame Yeye Ambaye ni yeye yule jana na leo, na hata milele; na Ambaye habadiliki katika tabia Yake ama katika njia Zake. Ambapo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Lake, Huyo hapo katikati yao! Na si katikati yao tu kama anayependezwa kutazama tu bila kuhusika, ama kama malaika mwandishi; bali Yuko hapo amesimama akionyesha hasa Yeye ni nani - Uzima na Mtegemezaji na Mpaji wa vipawa vyote vyema kwa kanisa. Haleluya!

*"Yeye aendaye katikati ya vinara vya taa saba vya dhahabu."* Jinsi maneno hayo yalivyo na maana yanapoangaliwa katika nuru ya Maandiko, ambayo yanamweleza Yeye kama "Kristo Aliye Uzima wetu." Kwa kuwa Kristo, hakika, Ndiye uzima wa kanisa. Kanisa halina uzima mwingine. Bila Yeye hilo ni shirika tu la kidini, klabu, kusanyiko la watu lisilo na maana. Kama vile maiti iliyopambwa kwa lulu na kuvalishwa ingali ni maiti, vivyo hivyo na kanisa, haidhuru mipango na jitihada zake za fadhili zingefanikisha nini, bila Kristo hilo ni maiti pia. Lakini Yeye akiwa yuko katikati yake, Yeye akilitia moyo, linakuwa kwa mshangao wa wote "Mwili Wake, utimilifu Wake Yeye anayejaza vyote katika yote." Na saa hii hii Yeye anatembea katikati ya kinara cha taa cha dhahabu cha wakati wa mwisho. Vile alivyokuwa wakati alipotembea katika wakati wa kwanza ndivyo alivyo hata sasa katika wakati huu wa mwisho. Yesu Kristo YEYE YULE, JANA, na LEO, na HATA MILELE.

*"Vinara vya taa saba vya dhahabu."* Katika Kutoka 25:31, inasema,

*"Nawe fanya kinara cha taa cha dhahabu SAFI; hicho kinara na kifanywe cha kazi ya KUFUA; tako lake, na mti wake, vikombe vyake, na matovu yake, na maua yake, vyote vitakuwa vya kitu kimoja nacho."*

Kanisa la kweli la Yesu Kristo, bibi-arusi, linafananishwa na dhahabu SAFI. Haki ya Bibi-arusi ni haki YAKE Yesu. Sifa za bibi-arusi ndio sifa Zake Mwenyewe zenye utukufu. Kitambulisho chake bibiarusi kinapatikana katika Yeye. Kile alicho Yeye, bibi-arusi anapaswa kukionyesha. Kazi azifanyazo Yeye, bibi-arusi anapaswa kuzionesha. Hakuna dosari ndani yake bibi-arusi. Yeye ana utukufu wote ndani na nje. Tangu mwanzo hadi mwisho yeye ni kazi ya Bwana wake, na kazi Zake zote ni kamilifu. Kwa kweli ndani yake kumejumlishwa na kudhihirishwa hekima ya milele na kusudi la Mungu. Mtu atatambuaje jambo hilo? Mtu anawezaje kulielewa? Ingawa hatuwezi kufanya jambo hilo, tunaweza kulikubali kwa imani, kwa maana Mungu amelinena.

Lakini si kwamba tu kinara hicho cha taa ni cha dhahabu, ni cha dhahabu ya KUFUA. Kimetengenezwa kwa mikono kwa dhahabu ya kufua, kulingana na maelezo yake yaliyotolewa na Roho. Nje ya Bwana na Mwalimu wake, Yesu Kristo, je! kuna watu waliopata kupigwa na kutakaswa kama bibi-arusi wa Yesu Kristo? Hakika anayatimiza mateso ambayo Kristo aliacha. Ananyang'anywa mali zake. Maisha yake yamo hatarini. Anahesabiwa kama kondoo wa kuchinjwa. Anauawa siku nzima. Anateseka sana, lakini katika hayo yote yeye hajilipizi kisasi, wala hasababishi wengine wateseke. Anayestahili Injili ni bibi-arusi huyu wa kupendeza wa Kristo. Na kama vile dhahabu inavyofulika, ambapo shaba itavunjika ikifuliwa, dhahabu hii ya Mungu itastahimili mateso yake kwa ajili ya Bwana, si kukunjwa, si kuvunjwa, si kuhabiriwa, bali kufanywa kitu chenye uzuri na furaha milele kwa majaribu na majaribio ya maisha haya.

**KRISTO ANAWASIFU WALIO WAKE**

Ufunuo 2:2,3,

*"Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya: tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo;*

*Tena ulikuwa na subira, na kuvumilia, na umekuwa na bidii kwa ajili ya Jina Langu, wala hukuchoka.*"

Jinsi Mwokozi anavyowasifu na kuwapongeza watoto Wake kwa uzuri. Anatoa hesabu kamili ya misimamo yao mizuri ya kiroho na tabia yao. Anajua ya kwamba kuna udhaifu kati yao, lakini hata hivyo haukemei. Je! hilo si ni kama Bwana tu? Yeye anajua jinsi ya kututia moyo katika mambo mazuri na kutuzuia kufanya mabaya. Sote tungejifunza somo zuri papa hapa katika kulea kanisa na familia zetu. Na bora zaidi, sote tungeweza kujifunza somo zuri katika jambo hilo kwamba Mungu hushughulikia kila mmoja

wetu namna hii hii kabisa. Kamwe usife moyo, Mtakatifu wa Mungu, kwa maana Mungu si asiye na shukrani kusahau matendo yenu ya upendo. Lolote tunalofanya, hata kumpa mtu kikombe cha maji baridi, kuna thawabu na baraka kutoka kwa Bwana.

*"Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako." Anapotembea katikati ya kanisa Lake, Yeye anajua mateso ya watu Wake, na anashughulika.* Kama ilivyokuwa katika siku za utumwa kule Misri wakati aliposikia vilio vyao, Yeye asiyebadilika angali anasikia vilio vya wanaoteseka wakati anapotembea kati yao. Neno lenyewe, taabu, linaonesha uchovu unaotokana na kugandamizwa. Watu wa Mungu hawamfanyii kazi tu katika taabu ya upendo, bali wanateseka kwa ajili Yake kwa furaha. Wao ni wavumilivu katika kuibeba ile nira. Wakati huu wa kwanza ulipata mateso mengi. Ilibidi wakati huu ufanye kazi kwa bidii kuhubiri Injili na kueneza kweli. Wito wao mkuu maishani ulikuwa ni kumtumikia Mungu, na wakati matumaini yao katika maisha yalipokwisha wao walikuwa na subira na wakakabidhi yote Kwake Ambaye alikuwa ameahidi malipo yadumuyo mbinguni kwa ajili ya yale waliyopoteza kwa ajili Yake duniani.

Nafikiri tunapaswa kusimama hapa na kushughulikia wazo kwamba watu wa Mungu daima wameteswa na daima watateswa. Unajua kwamba Mwanzo ni kitabu cha mianzo, na kile unachoona kilianza pale kitaendelea moja kwa moja mpaka Ufunuo wala hakitabadilika. Hapo tunaona ya kwamba Kaini alimtesa na kumwua Habili kwa sababu yule wa pili alimpendeza Mungu. Ndipo tunaona picha kamilifu ya mwana wa Ibrahimu katika mwili, Ishmaeli, aliyemchokoza na kumpiga mwana wa ahadi, Isaka. Na kulikuwa na Esau, ambaye alimchukia Yakobo na angemwua, kama Mungu asingeingilia kati. Katika Agano Jipya tunamwona Yuda akimsaliti Yesu, ambapo mashirika ya kidini katika karne ya kwanza yalijaribu kuwaangamiza wale waamini wa mwanzoni. Wana wa ulimwengu huu, wanaoongozwa na ibilisi, wanawachukia watoto wa Mungu wanaoongozwa na Roho.

Haidhuru Mkristo ni mwenye haki na mwaminifu jinsi gani mbele ya watu, na haidhuru ni mwenye fadhili jinsi gani kwa mwanadamu mwenzake, akifanya tu yaliyo mema, hebu amkiri Kristo kama Mwokozi wake na akiri kutenda kazi kwa karama za Roho Mtakatifu katika lugha, unabii, kuponya na miujiza, bado atalaumiwa. Roho ya ulimwengu huu inaichukia Roho ya Mungu, na kwa kuwa haiwezi kuishinda Roho ya Bwana inajaribu kukiangamiza chombo ambamo Roho wa Kweli anakaa.

Mateso na majaribu ni sehemu ya maisha ya binadamu, na fungu la maisha ya Mkristo. Kuna jambo moja tu unaloweza kufanya kuhusu hayo. Yakabidhi yote kwa Mungu, usihukumu, nawe umwachie Yeye kuyatatua na kufanya uamuzi wa mwisho.

*"Huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo."* Hawa Waefeso waliamini ya kwamba watu wa Mungu wanapaswa kuwa watakatifu. Kulingana na aya hii walichukua hatua kuuweka mwili usichachushwe na dhambi. Ni wazi kabisa ukengeufu ulikuwa umeanza tayari. Dhambi ilikuwa imeingia kanisani. Lakini wao walikuwa watiifu kwa maneno ya Paulo aliposema wawaondoe watu waovu kati yao. Walikuwa ni watu waliotengwa. Walikuwa wametoka katika ulimwengu, na sasa hawangeweza kuuruhusu ulimwengu uingie kati yao. Wasingevumilia dhambi kanisani. Utakatifu haukuwa ni mazungumzo tu kati yao au msemo; ulikuwa ni maisha.

*"Umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo."* Jamani, huo ni msemo wa kukata. "Umewajaribu wale wanaojiita mitume." Je! hilo silo jambo la ujasiri? Watu wana haki gani kuwajaribu wale wanaojiita mitume? Nao wanawajaribuje? Loo, napenda jambo hili. Hili hapa katika Wagalatia 1:8,

> *"Lakini ijapokuwa sisi, au malaika wa mbinguni, atawahubiri ninyi Injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe."*

Mitume ndio waliowaletea watu Neno halisi la asili. Hilo Neno la asili halingeweza kubadilika, hata doti au kimstari chake. Paulo alijua Mungu ndiye aliyekuwa amenena naye, kwa hiyo akasema, "Hata kama mimi nikija na kujaribu kutoa ufunuo wa pili, kujaribu kufanya badiliko moja dogo katika yale niliyotoa hapo kwanza, na nilaaniwe." Mnaona, Paulo alijua ya kwamba ufunuo wa kwanza ulikuwa sahihi. Mungu hawezi kutoa ufunuo wa kwanza, kisha ufunuo wa pili. Kama angefanya hivyo, angekuwa akibadilisha nia Yake. Yeye anaweza kutoa ufunuo, kisha auongezee, kama alivyofanya katika Bustani ya Edeni wakati alipomwahidi mwanamke Uzao, halafu baadaye akasema huo Uzao ulibidi uje kupitia kwa Ibrahimu, na halafu baadaye akasema ungekuja kwa ukoo ule ule katika Daudi. Lakini ulikuwa ni ufunuo ule ule. Uliwapa tu watu habari zaidi kuwasaidia waupokee na kuufahamu. Lakini Neno la Mungu haliwezi kubadilika. Ule Uzao ulikuja hasa kama ulivyofunuliwa. Haleluya. Na angalia kile hao mitume wa uongo walikuwa wakifanya. Walikuja na neno lao wenyewe. Hao Waefeso walijua Neno hilo kama Paulo alivyolifundisha. Walikuwa wamejaa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya Paulo. Waliwaangalia wale mitume wa uongo machoni na kusema, "Hamsemi yale Paulo aliyosema. Kwa hiyo ninyi ni waongo." Loo, hilo linawasha moto moyo wangu. Rudini kwenye Neno! Kwa kweli si wewe unayemjaribu huyo mtume, na nabii na mwalimu, NENO NDILO LINALOWAJARIBU. Moja ya siku hizi atakuja nabii kwa Wakati wa Kanisa la Laodikia nawe utajua kama yeye ni yule wa kweli aliyetumwa kutoka kwa Mungu ama si wa kweli. Naam utajua, kwa kuwa kama yeye ni wa Mungu ATAKUWA KATIKA HILO NENO SAWASAWA NA VILE MUNGU

ALIVYOMPA PAULO. YEYE HATATOKA KWENYE NENO HILO HATA KIDOGO, HATA KWA NUKTA MOJA. Katika wakati huo wa mwisho, kutakapotokea manabii wengi wa uongo, angalia na uone jinsi wanavyokazana kukwambia ya kwamba kama huwaamini wao pamoja na yale wanayosema, utapotea; lakini wakati yule NABII WA SIKU YA MWISHO atakapojitokeza, kama yeye kweli ni nabii huyo, atakuwa akipiga kelele, "Rudini kwenye Neno la sivyo mmepotea." Yeye hatajenga kwenye ufunuo wa kibinafsi ama fasiri, lakini kwenye Neno. Amina, na Amina!

Hawa mitume wa uongo ni mbwa mwitu wakali ambao Paulo alinena habari zao. Alisema, "Mara nikiondoka, wao watajaribu kuja na kudai ufunuo sawasawa na wangu; lakini kusudi lao si kuwasaidia, bali ni kuwaangamiza." Matendo 20:27-32,

> *"Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.*
>
> *Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa Lake Mungu, alilolinunua kwa damu Yake Mwenyewe.*
>
> *Kwa kuwa najua jambo hili, ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi.*
>
> *Tena katika ninyi wenyewe watainuka watu, wakisema mapotovu (neno lao wenyewe na mawazo yao, si ya Mungu) wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.*
>
> *Kwa hiyo kesheni, mkikumbuka, ya kwamba miaka mitatu usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi.*
>
> *Basi, ndugu zangu, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa Neno la neema Yake, ambalo laweza kuwajenga, na kuwapa urithi miongoni mwao wote waliotakaswa."*

Yohana aliyajua, pia, kwa kuwa alisema katika I Yohana 4:1,

> *" … Manabii wengi wa uongo (tayari) wametokea ulimwenguni."*

Hiyo Roho ya mpinga-Kristo tayari ilikuwa ikijipenyeza kanisani, nayo ilikuwa ikifanya jambo hilo kwa kulipinga Neno. Mbona hapa ndipo yote yalipoanza. Papa hapa katika wakati wa kwanza wa kanisa. Tayari walikuwa wakilikana Neno na kuanzisha kanuni zao za imani na falsafa badala ya Neno. Huyo ni mpinga-Kristo, kwa maana Yesu ni Neno. Kuwa mpinga-Neno ni kumpinga Yesu. Kuwa mpinga-Neno ni kuwa mpinga-Kristo, kwa maana Roho na Neno ni MMOJA. Kama wewe ni mpinga-Neno, itakubidi kuwa mpinga-Kristo. NA KAMA ILIANZIA KATIKA KANISA LA KWANZA ITAPASWA KUKUA MPAKA MWISHO WAKATI ITAKAPOCHUKUA MAMLAKA. Na jambo hilo ndilo hasa utakaloona tunapopitia nyakati zote. Inaanza ikiwa mindogo sana katika Wakati wa Efeso na inakua katika kila wakati mpaka utaratibu wa mpinga-Neno, mpinga-Kristo, unachukua mamlaka kabisa na mamlaka isiyokosea ya Neno la Mungu inakataliwa na mitume wa uongo wa kanisa la uongo.

Sasa ni rahisi kuwa na wazo la makosa la yale tunayozungumzia kwa sababu ninalitamka jambo hili kwa uzito sana. Ingeweza kusikika kwako kama kwamba roho hii ya kupinga Neno, ya mpinga-Kristo ni kupinga katakata Neno, kukana Biblia kunakoishia katika kuikataa. Hapana bwana. Siyo hivyo. Kilicho, ni Ufunuo 22:18,19,

> *"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki.*
>
> *Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika kile Kitabu cha Uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki."*

Ni kubadilisha hata neno moja tu kwa kuondoa au kuongeza kwake. Ni hila ya asili ya Shetani katika Bustani ya Edeni. Yeye aliongezea tu neno moja dogo kwenye yale Mungu aliyokuwa amesema. Hilo lilitosha. Lilileta mauti na maangamizi. Na huko Efeso, ilikuwa ni vile vile. Neno tu lililoongezwa, neno tu lililoondolewa, na mpinga-Neno, roho ya mpinga-Kristo ikaanza kustawi.

Mlilipata sasa? Kuna wale mapacha tena. Kuna hiyo miti miwili tena, inayokua pamoja katika ardhi ile ile, ikila chakula kile kile, ikinywa katika mvua ile ile, na kufaidika na jua lile lile. Lakini wanatokana na mbegu TOFAUTI. Mti mmoja UNALITII Neno la Mungu, sawasawa tu na vile Mungu alivyolitoa, na unalipenda na kulitii. Mti huo mwingine umetokana na mbegu ambayo inapinga Neno la Mungu na kulibadilisha po pote unapotaka. Unaweka kanuni zake wenyewe na mafundisho yake ya sharti badala ya Neno la kweli lililo hai kama tu vile alivyofanya Kaini, ambaye hatimaye alimuua Habili. Lakini msiogope enyi kundi dogo. Dumuni na Neno. Weka Neno hilo kati yako na ibilisi. Hawa hakufanya hivyo naye akashindwa. Na wakati kanisa linapoliacha Neno linaingia kwenye kilindi cha giza la Shetani.

*"Tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya Jina Langu, wala hukuchoka."* Hili ni karibu sawa tu na kama ilivyosemwa katika aya ya pili. Lakini katika aya ya pili kazi, taabu, na subira zilitokana na kulilinda Neno takatifu ambalo walikuwa wamepewa. Jinsi walivyowazuia maadui. Jinsi walivyokuwa sifa njema kwa Paulo. Lakini katika aya hii mateso yao na majaribu na subira yao ni juu ya Jina la Yesu lililobarikiwa.

Unajua hilo si jambo la ajabu hata kidogo, kwa maana ni Neno pamoja na Jina vinavyomleta adui atufurikie kama mafuriko. Hilo Neno lenye nguvu lililodhihirishwa katika kuponya kwingi, ishara nyingi, maajabu, na madhihirisho mengine, liliwafanya Mafarisayo kupaza sauti kwa ajili ya kifo cha waamini wa kweli. Na sasa Jina hilo, lililochukiwa na kudharauliwa na Wayahudi, linadhihakiwa na wastaarabu kama walivyocheka kuwazia mtu ye yote angeweza kuwa mjinga mno kumwamini mtu aliyekufa na kufufuka tena na ati na sasa anakaa mbinguni. Kwa hiyo hawa hapa wale wadhalimu wa kidini, Wayahudi, wakimlaani huyu Yesu, Ambaye kwao alikuwa ni Masihi wa uongo; na hapa walikuwako wale wengine wakilicheka kwa kufurahia sana na kulidhihaki kwa maneno machungu Jina la mungu mgeni, Ambaye kwao hakuwa mungu hata kidogo.

Sasa hapa pana jambo jingine lililoanza katika wakati ule na litaendelea moja kwa moja katika nyakati nyingi, likizidi kupata kina na kuzidi kuwa giza. Hiyo ni kusema, watu walikuwa wakilikataa Jina hilo. Haikuwa Kanisa la kweli la Efeso lililokuwa likifanya jambo hilo. Hapana bwana. Ilikuwa ni wale mitume wa uongo. Ilikuwa ni mtu wa nje akijaribu kuingia na kuwachafua waamini. Waefeso walijua Jina hilo na kulipenda. Kumbuka asili ya Kanisa hilo la Efeso. Kundi dogo la watu waliokuwa wakimtazamia Masihi walisikia ya kwamba nabii aliyejiita mtangulizi wa Masihi alikuwa ametokea katika jangwa la Palestina na alikuwa akiwabatiza watu wapate kutubu dhambi zao. Hawa, basi, walipokea ubatizo wa Yohana. Lakini wakati Paulo alipowajia aliwaonesha ya kwamba huyo nabii amekufa, ya kwamba Yesu alikuwa amekuja na kutimiza maisha Yake kama dhabihu kwa ajili ya dhambi, na ya kwamba SASA Roho Mtakatifu alikuwa amekuja na angeingia na kuwajaza waamini wote wa kweli katika Yesu, yule Masihi. Waliposikia haya, WALIBATIZWA KWA JINA LA BWANA YESU, na Paulo alipoweka mikono yake juu yao, wote wakajazwa na Roho Mtakatifu. Walijua kutii Neno ni nini, kubatizwa katika Jina Lake (Bwana Yesu Kristo) na kwa njia hiyo wao walijua wangejazwa na Roho Mtakatifu. Usingeweza kuwafanya watu hao wabadilike. Walijua kweli. Matendo. 19:1-7.

Walijua nguvu za Jina hilo. Wao walijua nguvu za hilo Jina. Waliona ya kwamba hilo Jina lilikuwa na nguvu sana kwamba hata leso zilizotolewa kutoka katika mwili wa Paulo na zikatumwa katika Jina la Yesu kwa watu waliokuwa wanaumwa zingewaponya wagonjwa kutokana na kila namna ya magonjwa na kutoa pepo wachafu. Jina hilo lilitenda kazi dhahiri sana hata Wayahudi wapotovu kule Efeso walijaribu kulitumia kupunga pepo. Matendo 19:11-17,

> *"Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida;*
>
> *Hata wagonjwa wakaletewa leso na nguo zilizotoka mwilini mwake, magonjwa yao yakawaondokea, pepo wachafu wakawatoka.*
>
> *Basi baadhi ya Wayahudi wenye kutanga-tanga, nao ni wapunga pepo, wakajaribu kutaja Jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu, wakisema, Tunawaapisha kwa Yesu, Yule anayehubiriwa na Paulo.*
>
> *Walikuwako wana saba wa mtu mmoja Skewa, Myahudi, mkuu wa makuhani, waliofanya hivyo.*
>
> *Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua, na Paulo namfahamu; lakini ninyi ni nani?*
>
> *Na yule mtu aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili, akawaweza, akawashinda, hata wakatoka mbio katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa.*
>
> *Habari hii ikajulikana na Wayahudi wote na Wayunani pia waliokaa Efeso; hofu ikawaingia wote, na Jina la Bwana Yesu likatukuzwa."*

Wao walijua maisha yenye haki yaliyoambatana na mtu kulichukua Jina hilo, kwa maana kila anayelitaja Jina la Bwana, na aache dhambi. Mwe watakatifu, enyi mnaovibeba vyombo vya Bwana. Usilitaje Jina la Bwana Mungu wako bure. Hawa Waefeso walikuwa WAKRISTO. Walichukua Jina, na Jina hilo lilikuwa ni Kristo, ambaye alikuwa ni Roho wa Mungu ndani yao, na Ambalo lilikuwa moja ya Majina matatu ya Bwana wao.

*"...Tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya Jina Langu, wala hukuchoka."* Hawa waamini hawakuwa wakivumilia kwa ajili ya Paulo, ama kwa ajili ya madhehebu fulani. Wao hawakuwa wameshikilia miradi na mashirika ambapo walijenga viwanja vya biashara. Walimtumikia Bwana. Walikuwa watumishi Wake, si vibaraka vya madhehebu. Wao hawakuenda kanisani Jumapili na kuzungumzia habari za Jina hilo kisha walisahau siku zilizosalia za juma. Wao hawakulitumikia Jina hilo kwa mdomo tu. Hapana Bwana.

Wao walitoa maisha yao.

Yote waliyofanya, walifanya katika Jina hilo. Katika Jina hilo walitenda, lakini kama wasingeweza kutenda katika Jina hilo, basi walijiepusha na kutenda. Hawa walikuwa Wakristo waliowekwa mbinguni ambao tabia zao zilikuwa katika Bwana.

Lakini kundi hilo la mzabibu wa uongo lililotaka kuliharibu Jina hilo lilikuwa tayari kama mbwa mwitu anayejificha gizani, likingojea kuingia na kurarua. Lakini hao watakatifu walistahimili majaribu nao wakashikilia Neno hilo pamoja na Jina.

**LALAMIKO LA MUNGU**

Ufunuo 2:4,

*"Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza."*

Ili kufahamu jambo hili huna budi kutambua ya kwamba Roho haneni na wale watakatifu wa kwanza wa Efeso peke yao. Ujumbe huu ni kwa ajili ya wakati wote mzima uliodumu kwa muda wa kama miaka 120. Ujumbe wake, basi, ni kwa vizazi vyote katika kipindi hicho. Sasa historia inafululiza kujirudia yenyewe. Katika vizazi vya Israeli tunaona ufufuo katika kizazi kimoja, lakini tunaona mioto ikififia katika kizazi kinachofuata. Katika kizazi cha tatu, makaa ya moto huenda yanameka kidogo, lakini katika cha nne huenda kusiwe na dalili ya mabaki-mabaki hata kidogo ya ule mwali wa mwanzoni. Basi Mungu anauwasha moto tena, halafu tendo lile lile linarudiwa. Ni dhihirisho la kweli kwamba Mungu hana wajukuu. Wokovu haupokezanwi kwa kuzaliwa kimaumbile kama kusivyo na ukweli hata kidogo wa uhalifa wa kimitume. Haliko katika Neno. Unaanza na waamini waliozaliwa kweli mara ya pili, na wakati kizazi kinachofuata kinapokuja wao si Wakristo wa kweli tena, lakini wamechukua jina la kimadhehebu na sasa wao ni Wabatisti, Wamethodisti, na kadhalika. Hivyo ndivyo walivyo hasa, pia. Wao si Wakristo. Huna budi kuzaliwa kwa mapenzi ya Mungu, si mapenzi ya mwanadamu, upate kuokolewa. Lakini jamaa hawa wote wanaungana sasa kwa mapenzi ya mwanadamu. Sisemi ya kwamba wengine wao hawako sawa na Mungu. Sisemi hivyo hata kidogo, lakini ule moto wa kwanza umezima. Wao hawako vile walivyokuwa tena.

Ile shauku kali ya kumpendeza Mungu, shauku ya kutaka kulijua Neno Lake, kilio cha kumtafuta Roho, yote yanaanza kufifia na badala ya kanisa hilo kuwaka kwa moto wa Mungu, limepoa na kuwa la kawaida kidogo. Hilo ndilo lililokuwa likitendeka kule nyuma kwa Waefeso. Walikuwa wakiwa wa kawaida kidogo. Kule kujikana kwao kwa ajili ya Mungu kulikuwa kunafifia na watu hawakujali sana yale Mungu aliyowawazia kwa kuwa walianza kujali yale ulimwengu ulichowawazia. Kizazi hicho cha pili kilichokuja kilikuwa tu kama Israeli. Walitaka wawe na mfalme kama mataifa mengine. Walipofanya hivyo, walimkataa Mungu. Lakini walifanya hivyo hata hivyo. Hiyo ndiyo historia ya kanisa. Wakati linapowazia zaidi juu ya kufanana na ulimwengu badala ya kufanana na Mungu, haichukui muda mrefu kabla hujawaona wakiacha kufanya mambo waliyozoea kufanya, na kuanza kufanya mambo ambayo wao wasingeyafanya hapo awali. Wanabadilisha mtindo wao wa kuvaa, mitazamo yao na tabia zao. Wanakuwa walegevu. Hiyo ndiyo maana ya "Efeso": kulegea—kuteleza.

Mzunguko huo wa ufufuo na mauti haujafa kamwe. Unalohitaji kufanya tu ni kukumbuka tukio hili lililopita la Mungu katika Roho wakati wanaume na wanawake walipovalia kama Wakristo, walienda kanisani, wakaomba usiku kucha, wakaenda pembeni mwa barabara nao hawakuonea haya kuhusu madhihirisho ya Roho. Waliyaacha makanisa yao ya kale yaliyokufa na kuabudu nyumbani ama kwenye majengo ya maghala ya kale. Walikuwa na kitu halisi. Lakini haikuchukua muda mrefu sana hata walipoanza kupata pesa za kutosha kujenga makanisa mazuri mapya. Waliweka kwaya badala ya wao wenyewe kumwimbia Mungu. Waliwavalisha wana kwaya majoho. Waliunda mashirika na wakayaongoza kwa njia ya mwanadamu. Mara wakaanza kusoma vitabu visivyostahili kusomwa. Waliacha milango wazi na mbuzi wakaingia na kutawala. Kilio cha furaha kilikwisha. Uhuru wa Roho ulikuwa umekwisha. Loo! waliendelea na desturi; lakini ule moto ulikuwa umezimika na weusi wa majivu ndio karibu tu uliobakia.

Muda kidogo uliopita nilisema ya kwamba Yohana alifahamu kumpenda Mungu ni kitu gani. Huyo mtume mashuhuri wa upendo bila shaka angeona jambo hilo wakati kanisa lilipoanza kupoteza upendo huo wa kwanza wa Mungu. Katika I Yohana 5:3, yeye anasema,

*"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri Zake (Neno Lake)."*

Kuchepuka kidogo kutoka kwenye Neno hilo kulikuwa ni hatua moja kutoka kwa Kristo. Watu wanasema wanampenda Mungu, wanaenda kanisani, hata wanapiga makelele na kufurahi na kuimba na kuwa na wakati wa furaha wa kuchemka. Lakini hayo yote yanapokwisha, wewe angalia uone kama wako kwenye hilo NENO, wakienenda katika hilo, wakiishi ndani yake. Kama wakipitia katika hayo mengine yote na kisha wasiende katika Neno hilo, wanaweza kusema wanampenda Mungu bali maisha yao yanasimulia hadithi nyingine. Sijui kama Yohana hakuona mengi ya hayo kabla hajafa; watu wakisema walimpenda Mungu lakini hawalitii Neno Lake. Loo! Kanisa la Efeso, jambo fulani limewapata. Mtu fulani anajaribu

aidha kuongeza kwenye Neno hilo ama kuondoa kwake. Lakini wanalifanya kwa hila sana hata huwezi kuliona. Hawajafanya tendo kubwa sana hata uweze kuliona huko nje waziwazi. Limejificha, na wanalileta kwa njia ya hoja na ufahamu wa kibinadamu na litashinda labda mlikatae. Rudini Pentekoste kabla ya kuchelewa!

Lakini kama kawaida watu hawatii onyo la Mungu. Huo moto wa ufufuo uliowashwa juu ya Neno takatifu ni mzuri sana, na dhihirisho la Roho limebarikiwa sana, hivi kwamba uoga mdogo unapenya ndani na mnong'ono moyoni unasema, "Tunawezaje kuilinda kweli tuliyo nayo? Tunaweza kufanya nini kuona ufufuo huu ukiendelea?" Hapo ndipo roho ya "mpinga-Kristo" inapoingia na kunong'oneza, "Angalia, mnayo ile kweli sasa, angalieni isipotee. Undeni madhehebu na mworodheshe kanuni zenu za imani mnazoamini. Ziandikeni zote katika mwongozo wa mafundisho ya kanisa." Nao wanafanya hivyo. Wanaunda madhehebu. Wanaongeza kwenye Neno. Nao wanakufa kama tu Hawa alivyofanya kwa kuchukua Neno moja lisilo sahihi. Neno la Mungu ndilo huleta uhai. Na si yale tunayosema kuhusu Neno yaliyo muhimu, bali ni yale Mungu aliyosema.

**ONYO LA MUNGU**

Ufunuo 2:5,

*"Basi kumbuka ni wapi ulikoanguka, ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza; lakini, usipofanya hivyo naja kwako upesi, Nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu."*

Mungu anawaambia WAKUMBUKE. Ni dhahiri kitu fulani kilikuwa kimewaacha akili zao. Walikuwa wamesahau kitu fulani. Aliwaambia warudi nyuma katika nia zao mahali pao pa asili. Chimbuko la wakati wa kwanza lilikuwa ni Pentekoste. Walikuwa wameanguka kutoka hapo. Walikuwa wamesahau utukufu na maajabu yake. Ilikuwa ni wakati wa kurudi nyuma katika nia zao na halafu katika hali halisi. Kurudi wakati walipoweza kusema, "Kwangu mimi kuishi ni Kristo." Kurudi nyuma kwenye usafi wakati Anania na Safira walipoadhibiwa. Warudi kwenye Mlango uitwao Mzuri. Loo! ni jambo la aibu jinsi gani kuondoka kwa Mungu na kuyapenda matendo yale yanayolichafua Jina Lake. Hebu hao wanaoliitia Jina Lake waache dhambi na kuweka vyombo vyao safi kwa ajili ya Mungu. Angalia kile ulichokuwa wakati mmoja moyoni mwako, na nia yako, na katika maisha yako. Halafu rudini kwake.

Na njia ya kurudi ni ipi? Njia hiyo ndiyo njia ya toba. Kama mwenye dhambi hana budi kumjia Mungu kwa njia ya toba basi mwenye uvuguvugu ama aliyerudi nyuma hana budi kutubu namna hiyo hiyo na zaidi sana. Tubuni! Zaeni matunda yanayopatana na toba. Lithibitishe kwa maisha yako. "Usipotubu," Mungu alisema, "Nitakiondoa kinara chako." Hakika. Kanisa katika hali hiyo haliwezi kutoa nuru kwa ulimwengu. Nuru yake imegeuka kuwa giza. Mungu basi atamwondoa mjumbe wake mwaminifu na wachungaji wake waaminifu na kuwaacha peke yao, nao wataendelea kuongea juu ya Ukristo, lakini wawe hawanao.

Tubu upesi! Usisite! Kwa dhahiri, Efeso ulisitasita, kwa kuwa kipindi chake cha maisha hakikuwa kirefu sana. Utukufu wa Mungu ulipungua upesi sana. Haikupita muda mrefu ule mji ukaangamizwa. Lile hekalu lake la fahari likawa magofu matupu yasiyo na umbo. Ardhi ikawa bwawa walimoishi ndege wa majini; idadi kubwa ya watu iliangamia kuacha wasioamini wachache walioishi katika kijiji kichafu sana. Hakukuwa na hata Mkristo mmoja aliyesalia. Taa iliondolewa mahali pake.

Sasa haimaanishi ya kwamba huo haungeweza kutubu. Haimaanishi ya kwamba hatuwezi kutubu. Tunaweza. Lakini lazima iwe haraka. Haina budi kuwa ni kilio cha kweli cha Mungu toka moyoni katika masikitiko, na ndipo Mungu atarejesha. Utukufu utakuja tena.

**MBEGU YA UNIKOLAI**

Ufunuo 2:6,

*"Lakini unalo neno hili, kwamba wayachukia matendo ya Wanikolai, ambayo na Mimi nayachukia."*

Sasa kuna mawazo mawili juu ya kile Wanikolai walikuwa. Inasemwa na baadhi ya wengine ya kwamba walikuwa ni kundi la makafiri lililokuwa na mwanzilishi wao, Nikolasi wa Antiokia, mwongofu, aliyekuwa mmoja wa wale mashemasi saba wa Yerusalemu. Walikuwa na sikukuu za kipagani nao walikuwa na mienendo michafu sana. Walifundisha ya kwamba ili kushinda mambo ya tamaa za mwili kabisa itamlazimu mtu kujua kwa vitendo mapana na marefu yake kwanza. Ilibidi basi watoe nafasi kwa tamaa za mwili hivi kwamba uasherati wao ukamilishwe. Hivyo basi waliwapa majina mawili ya Agano la Kale ambayo yanawakilisha wenda wazimu wa jinsi hiyo: Balaamu na Yezebeli. Kwa kuwa Balaamu aliwapotosha watu na hivyo basi akawashinda, ilisemekana ya kwamba Nikolasi alifanya vivyo hivyo. Kundi hili linadhaniwa kwamba lilifukuzwa Efeso ndipo likapata mahali pa kukaa huko Pergamo.

Lakini shida kuhusu imani hii ni kwamba si kweli. Hakuna historia kabisa ya jambo hilo. Ni mapokeo

mazuri sana. Kuwa na maoni kama hayo ni kuufanya wakati wa kanisa la Efeso kuwa wa kihistoria kabisa, usio na uhusiano wo wote na siku hizi. Hii si kweli, kwa maana cho chote kinachoanza katika kanisa la mwanzoni hakina budi kuendelea katika kila wakati mpaka hatimaye kikabarikiwe na kuinuliwa na Mungu ama kuangamizwa kama kitu kichafu katika ziwa la moto. Kwamba mapokeo haya kweli ni kinyume cha Maandiko, angalia tu kwamba katika Ufu. 2:2, Kanisa la Efeso HALIKUWEZA KUCHUKULIANA na watu wabaya. Kwa hiyo ilibidi wawafukuze, ama haingekuwa na maana kusema wasingeweza kuchukuliana nao. Kama hawakuwafukuza, basi walikuwa wakichukuliana nao. Sasa katika aya ya sita, inasema ya kwamba wao waliyachukia matendo yao. Kwa hiyo kundi hili la Wanikolai lilibakia kuwa sehemu ya wakati wa kwanza, wakiendelea na matendo yao. Hayo matendo yalichukiwa, lakini nguvu waliokuwa nazo hao watu hazikuondolewa. Hivyo tunaona mbegu katika kipindi cha Efeso ambazo zitaendelea na zitakuwa fundisho litakaloendelea mpaka, na katika, ziwa la moto.

Hawa Wanikolai ni akina nani? Neno hilo linatokana na maneno mawili ya Kiyunani. *Nikao*, ambalo maana yake ni kushinda, na *Laos*, ambalo maana yake ni washirika. Kwa kweli iliyo dhahiri, mtu fulani alikuwa akifanya jambo fulani katika kanisa lile la mwanzoni ambalo lilikuwa likiwatiisha washirika. Kama washirika walikuwa wakitiishwa, basi hapana budi ilikuwa ni "mamlaka fulani" iliyokuweko inafanya jambo hilo.

Ni kitu gani ambacho Mungu alichukia ambacho kilikuwa kinatendeka katika kanisa hilo? Yale yaliyokuwa yakiendelea wakati huo, na hivi sasa yanaendelea leo, ndiyo maana hasa ya neno Unikolai. Watu walikuwa kwa namna fulani wakiwekwa chini ya mamlaka fulani ambayo ilikuwa kinyume kabisa na Neno la Mungu.

Sasa ili kupata maana kamili ya yale tunayokaribia kuingilia, sina budi kuwatahadharisha mweke daima moyoni ya kwamba dini (mambo ya kiroho ukitaka), ina sehemu mbili ambazo zimesokotana bali zinahitilafiana kabisa kama nyeusi na nyeupe. Dini na ulimwengu wa roho vimefanyizwa kwa miti hiyo miwili ambayo mizizi yao ilikuwa huko Edeni. Mti wa Uzima na pia Mti wa Kujua Mema na Mabaya ilisimama katikati ya ile bustani na hapana shaka matawi yake yasokotana. Hivyo basi katika Kanisa lile la Efeso kuna kitendawili kile kile. Kanisa linaundwa na wema na wabaya. Kanisa linaundwa na Mizabibu miwili. Mizabibu hiyo iko kama ngano na magugu, vikikua pamoja. Lakini mmoja ni wa KWELI. Huo mwingine ni wa UONGO. Sasa Mungu atasema NA kila mmoja na atazungumza KUHUSU kila mmoja wao. Yeye ataiita kanisa. Na wateule peke yao ndio watakaojua yakini Roho wa kweli ni yupi. Ni wateule pekee ambao hawatadanganywa. Mathayo 24:24,

> *"Kwa maana watatokea Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; kiasi kwamba wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule."*

Kwa hiyo huko nyuma mbali sana katika kanisa la mwanzoni (kipindi kidogo sana baada ya Pentekoste) mzabibu wa uongo ulijisokotea kwenye Mzabibu wa Kweli nasi tunaona matendo haya ya Wanikolai. Na roho huyo ataonekana akiupiga vita Mzabibu wa Kweli mpaka wakati utakapoangamizwa na Mungu. Sasa mmelipata?

Sawa. Sasa hali ya kiroho ya kanisa hilo ilikuwa ni nini? Alikuwa ameuacha upendo wake wa kwanza. Kuacha upendo wake wa kwanza wa Neno la Mungu kulifunuliwa kwetu kama kuanguka kutoka kwenye ile asili yake, ambayo ilikuwa ni Pentekoste. Katika lugha rahisi, hilo linamaanisha kanisa hili lilikuwa katika hatari ya kuondolewa kutoka kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu, utawala wa Roho. Hili ndilo hasa lililotukia baada ya Musa kuwaongoza Israeli kutoka Misri. Njia ya Mungu ilikuwa kuwaongoza kwa wingu la moto, matamshi ya kinabii, miujiza na ishara, na maajabu yaliyotolewa na Mungu. Haya ilibidi yatimizwe na watu 'Walioteuliwa na Mungu', na 'Waliochaguliwa na Mungu', na 'Walioandaliwa na Mungu', na 'Waliotumwa na Mungu, na kambi nzima ikitawaliwa na nguvu za Roho Mtakatifu. Wao waliasi na kutaka orodha ya kanuni na kanuni za imani watakazoenenda kwazo. Ndipo walitaka mfalme. Halafu wakataka kuwa kama watu wa ulimwengu kabisa na wakaingia katika kukana imani kabisa na kutojali. Hivyo ndivyo jinsi hasa wakati wa kwanza wa kanisa ulivyoanza, na jambo hilo litaendelea kuharibika zaidi na zaidi, mpaka Roho Mtakatifu amekataliwa kabisa na Mungu hana budi kuwaangamiza watu.

Mnaona jinsi lilivyoanza katika kanisa la mwanzoni. Liliitwa matendo. Ndipo likawa fundisho. Likawa ndicho kielelezo. Ikawa njia isiyopinda. Hatimaye likashika hatamu na Mungu akasukumiwa kando. Loo! lilianza likiwa dogo sana, limetulia sana, bila shari kabisa. Lilionekana ni zuri sana. Lilionekana ni la kweli. Ndipo likashikilia, na kama vile chatu lililibana kanisa pumzi na kuua kiroho chote kilichokuwemo ndani yake. Loo, huo mzabibu wa uongo ni wa hila. Uko kama malaika wa nuru mpaka unakushika. Sasa nataka kusema ya kwamba ninaamini katika uongozi. Lakini si uongozi wa watu ninaouamini. Ninaamini katika uongozi wa Roho Mtakatifu akija kupitia Neno. Ninaamini pia, ya kwamba Mungu ameweka watu kanisani, watu ambao wana karama za Roho; nao wataliweka kanisa katika utaratibu. Ninaamini jambo hilo. Ninaamini pia ya kwamba kanisa linatawaliwa na watu ambao Mungu huwatuma kuchukua wajibu. Lakini uongozi huo ni KWA NENO, hivi kwamba si wanadamu kweli wanaoongoza bali ni ROHO WA MUNGU, kwa maana Neno na Roho ni MMOJA. Waebrania 13:7,

*"Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia Neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao."*

Lakini angalia kilichokuwa kinatendeka kule nyuma. Huo mzabibu wa uongo ulikuwa ukishikilia nao ulikuwa ukifundisha ya kwamba uongozi wa mwanadamu ulikuwa ni wa kweli. Ulifundisha ya kwamba lazima kanisa liongozwe. Ulifundisha usimamizi juu ya watu, lakini badala ya kulifanya jambo hilo katika njia ya Mungu, wao walichukua kwa urahisi tu mamlaka na kuweka mamlaka yote ya kiroho kwenye mikono yao wenyewe ndipo wakaja kutokea na ukuhani mtakatifu ukisimama kati ya Mungu na watu. Walirudi moja kwa moja nyuma kwenye utarativu wa kale wa Kiharuni. Wakawa mpinga-Kristo kwa maana waliondoa kazi Yake ya upatanisho Wake na kuweka wao. Mungu alichukia jambo hilo. Waefeso walilichukia hilo na mwamini ye yote wa kweli atalichukia pia. Ingetubidi tuwe vipofu kabisa tusiweze kuoana jambo lilo hilo likitenda kazi katika nyakati zote na sasa hivi limekuwa baya kupindukia. Jambo lenyewe lilikuwa, ni madhehebu. Hayo yaliwatenganisha watu. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa ni kitu kimoja. Kwa Roho MMOJA WOTE wamebatizwa kuwa mwili mmoja na KILA MMOJA hana budi kuongozwa na Roho Mtakatifu na KILA MMOJA anapaswa kushiriki katika kumwabudu Mungu. Lakini watu walitaka watawale wao, kwa hiyo wakachukua mamlaka, ndipo maaskofu wakawa maaskofu wakuu, na kwa vyeo vikubwavikubwa wakaliweka Neno la Mungu kando na kufundisha mafundisho yao wenyewe. Waliwafanya watu kuwatii wao mpaka ikafikia wakati ambapo njia yao ya kuabudia haikufanana kabisa na ya siku za mwanzoni baada ya Pentekoste. Matendo haya yalikuwa ndio mwanzo wa uhalifa wa kimitume. Kutoka kwenye uhalifa wa kimitume ilikuwa ni hatua moja rahisi na ya haraka kufikia "unachama wa kanisa" kama njia ya neema iokoayo. Neno liligeuzwa likawa kanuni ya imani. Mpinga-Kristo kwa roho yake alikuwa akilitawala kanisa.

Liangalie leo. Angalia jambo hilo leo. Ukisoma Matendo ya Mitume 2:4 jinsi wengine wanavyofanya, ungeweza kulisoma hivi, "Hata hapo ilipotimia siku ya Pentekoste, kukaja kasisi na mkate mdogo mwembamba na kusema, "Toa ulimi wako,' naye akaweka ule mkate mwembamba juu ya ulimi, na yeye mwenyewe akanywa divai kidogo na kusema, 'Sasa mmempokea Roho Mtakatifu'." Ati haiwezekani? Hapo ndipo kabisa Unikolai ulipofika. Wao wanasema, "Msijali vile Neno la Mungu lisemavyo. Huwezi kuelewa jambo hilo. Inabidi sisi tuwafasirie. Isitoshe Biblia haijamaliza bado. Haina budi kubadilika na wakati nasi tutawaambia hayo mabadiliko ni yapi." Jinsi jambo hilo lilivyo kinyume na Neno la Mungu ambalo linatamka kwa mkazo, "Mungu aonekane kuwa amini, na kila mtu mwongo," wakati wo wote panapotokea upinzani kwa ile kweli. Mbingu na nchi zitapita, lakini HAKUNA HATA NENO MOJA la Mungu litakaloshindwa. Kwa hiyo watu wanaongozwa na watu wanaodhania kuwa kitu wasicho. Wanasema ati wao ni badala ya Kristo, bali kile walicho ni mpinga-Kristo.

Hii hapa hadithi nyingine ya kusikitisha. Ni hadithi ya ubatizo wa maji. Katika siku za Yesu na baada ya Pentekoste wao walizamishwa katika maji. Hakuna mtu anayeweza kukana hilo. Watu wenye elimu wanasema ya kwamba jambo tu walilofanya ilikuwa ni kuwamwagia maji kwa sababu ilikuwa ni rahisi kupata vishimo vya maji katika sehemu nyingi. Na wakati wanapowamwagia maji, wanafanya jambo hilo kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, kama kwamba sifa hizo zilikuwa ni majina halisi, na kama kwamba kulikuweko na Miungu watatu badala ya mmoja tu. Lakini hebu kaa katika madhhebu hayo na ujaribu kuhubiri kweli ya kuzamishwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo nawe utafukuzwa. Usingeweza kuongozwa na Mungu na ukae mle ndani. Haiwezekani.

Sasa Paulo alikuwa ni nabii, alifundishwa na Roho Mtakatifu. Kama Paulo alibatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na akasema mtu ye yote aliyetenda tofauti na mahubiri yake amelaaniwa, basi wakati umefika wa kuamka na kuona ya kwamba kanisa haliongozwi tena na Roho Mtakatifu bali linaongozwa na Wanikolai. Matendo 20:27-30,

*"Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.*

*Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa Lake Mungu, alilolinunua kwa damu Yake Mwenyewe.*

*Kwa kuwa najua jambo hili, ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi.*

*Tena katika ninyi wenyewe watainuka watu, wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao."*

Paulo aliona jambo hilo likija. Lakini aliwaonya juu ya ukuhani huu wenye hila ambao ungekuja na kuchukua mamlaka kwa mafundisho yake ya uongo. Yeye alijua wangeanzisha njia ya ibada ambayo ingewazuia watu wasishiriki katika sehemu yo yote ya huduma ya Roho Mtakatifu. Na hata hivi leo kati ya wale wanaodai kuwa huru na wamejaa Roho hakuna uhuru mwingi sana katika wafuasi, na jambo zuri sana tunaloweza kuona ni wahubiri wachache wenye mahubiri yenye upako huku kundi limeketi pale tu na kujaribu kuyashika. Jambo hili liko mbali sana na Paulo aliyesema ya kwamba wakati wote wanapokutanika, wote walikuwa na uongozi wa Roho, na wote walishiriki katika ibada ya Kiroho.

Na jamii ya kanisa haijajifunza somo hili kutoka kwenye Maandiko wala kutoka kwenye historia. Kila wakati Mungu anapomwaga Roho Mtakatifu na watu wanakuwa huru, baada ya kitambo kidogo wao hujifunga tena kwenye jambo lile walimotoka. Wakati Luther alipotoka katika Ukatoliki, watu walikaa huru kwa muda kidogo. Lakini alipokufa, watu kirahisi tu waliyawekea utaratibu yale waliyodhania yeye aliyaamini pia wakaanzisha kanuni zao za imani na mawazo yao na wakajitenga na mtu ye yote aliyenena kinyume na yale waliyonena. Walirudi moja kwa moja kwenye Ukatoliki wakiwa na umbo tofauti kidogo. Na sasa hivi leo Waluteri wengi wako tayari kurudi huko nyuma kabisa.

Loo, naam! Katika Ufunuo 12, yule kahaba wa kale alikuwa na binti wengi. Hawa binti ni kama tu mama. Wao wanaliweka Neno kando, wanaikana kazi ya Roho wa Mungu, wanawatawala wafuasi, na wanalifanya kuwa jambo lisilowezekana kwa wafuasi kumwabudu Mungu isipokuwa waje kwa kupitia kwao ama kwa kupitia katika kielelezo chao, ambacho si kitu cho chote ila ni jama za kutokuamini kutoka kwa Shetani mwenyewe.

Tuko wapi, loo tuko wapi, kiroho? Tuko katika nyika ya giza. Ni umbali gani tumetangatanga kutoka kwenye kanisa la kwanza. Pentekoste haionekani popote na Neno haliwezi kupatikana. Uhalifa wa kimitume, ambao leo umejaa tele, haupo kwenye Neno. Ni chombo kilichobuniwa na watu. Unatangua isivyo halali ukweli kwamba MUNGU, WALA SI MWANADAMU, ameweka viongozi Wake kanisani. Petro hata hakuwa huko Rumi. Hata hivyo wanasema uongo na kusema alikuwa. Historia inathibitisha hakuwa. Kuna watu wanaosoma historia, lakini wanainua mabega yao na kurudi kuamini uongo. Unaweza kupata wapi 'aliye badala ya Kristo' katika Neno? Hakuna mtu anayepachukua mahali Pake, hata hivyo hilo limefanyika na watu wanalikubali. Ni wapi unapoweza kupata kwamba 'ufunuo ulioongezewa'unakubaliwa na Mungu, hasa sana ufunuo unaopingana na ule uliokwisha tolewa tayari? Hata hivyo wao wanaukubali na kuushikilia. Unapata wapi 'pegatore'? Unapata wapi misa? Unapata wapi 'kulipa pesa ili mtu apate kutolewa kutoka kuzimu'? Hakumo katika Neno, lakini watu huweka jambo hilo katika kitabu chao wenyewe na kwa njia hiyo wamewateka watu, wakiwatawala kwa hofu. Unapata wapi kwamba 'mwanadamu ana uwezo wa kutusamehe kana kwamba alikuwa Mungu'? "Mbwa mwitu wakali," hata si kali vya kutosha kuwaelezea. Unikolai. Madhehebu. Mwanadamu akimtawala mwanadamu.

Mrudieni Mungu. Tubuni kabla hamjachelewa. Tazama maandiko kwenye ukuta. Ni kuandika hukumu. Kama vile ambavyo vyombo vitakatifu vilivyotiwa unajisi na kwa hiyo vikaleta ghadhabu ya Mungu, sasa Neno takatifu limetiwa unajisi na Roho akahuzunishwa, na hukumu imekuja, hasa ipo mlangoni. Tubuni! Tubuni! Rudini Pentekoste. Rudi kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu. Rudini kwenye Neno la Mungu, kwa nini mfe?

## SAUTI YA ROHO

Ufunuo 2:7,

> *"Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa: Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya Mti wa Uzima, Ulio katika bustani ya Mungu."*

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."* Huenda ikawa kwamba mamilioni watasikia maneno haya au kuyasoma. Lakini ni wangapi watakaoyasikiliza? Hilo hatujui. Lakini yule atakayesikiliza na anayetaka kujua maneno ya kweli atamwona Roho wa Mungu akimtia nuru. Kama sikio lako liko wazi kwa Neno, Roho wa Mungu atalifanya Neno kuwa halisi kwako. Sasa hiyo ni kazi ya Roho. Ninaweza kukufundisha kweli, bali kama hufungui sikio lako upate kuisikia na moyo wako upate kuipokea, hutapata ufunuo

Sasa angalia, inasema ya kwamba Roho anazungumza na makanisa. Huo ni wingi, si umoja. Roho hakumfanya Yohana aandike haya kwa ajili ya kanisa la Efeso, wala kwa wakati wa kwanza tu. Ni kwa ajili ya nyakati zote za kanisa. Lakini hili ndilo kanisa la mwanzo. Na kwa hiyo ni kama Kitabu cha Mwanzo. Kile kilichoanza katika Mwanzo kinaendelea wakati wote katika Neno lote na hatimaye kinamalizikia katika Ufunuo. Kwa hiyo, kanisa hili linaloanza katika Matendo ndilo ramani ya Mungu kwa ajili ya nyakati zote mpaka linapoishia katika Wakati wa Laodikia. Liangalie kwa makini. Hebu kila wakati utahadhari, kwa maana kile kinachoendelea hapa ni mwanzo tu. Ule mti mdogo uliopandwa utakua. Utakua wakati wote katika zile nyakati. Huu, basi, ni ujumbe kwa kila Mkristo katika kila wakati mpaka atakapokuja Yesu. Naam, ndivyo ilivyo, kwa maana ni Roho anayenena. Amina.

## THAWABU ILIYOAHIDIWA

Ufunuo 2:7,

> *"...Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya Mti wa Uzima, Ulio katika bustani ya Mungu."*

Hii ndiyo thawabu ya usoni kwa washindi wote wa nyakati zote. Wakati wito wa mwisho wa kupiga vita umetangazwa, wakati silaha zetu zimekwisha kuwekwa chini, ndipo tutakapopumzika katika bustani ya Mungu na sehemu yetu itakuwa ni ule Mti wa Uzima, milele.

*"Mti Wa Uzima."* Huo si msemo unaopendeza? Umetajwa mara tatu katika Kitabu cha Mwanzo na mara tatu katika Kitabu cha Ufunuo. Katika sehemu zote sita ni mti ule ule na unaonesha kwa mfano kitu kile kile hasa.

Lakini mti wa Uzima ni nini? Vema, kwanza kabisa ingetupasa kujua mti wenyewe unawakilisha nini. Katika Hesabu 24:6, kama vile Balaamu alivyotoa sifa za Israeli, yeye alisema walikuwa "mfano wa mishubiri aliyoipanda Bwana." Miti katika Biblia nzima inanena juu ya watu, kama vile katika Zaburi 1. Hivyo basi Mti wa Uzima hauna budi kuwa ni Mtu wa Uzima, na huyo ni Yesu.

Sasa katika Bustani ya Edeni kulikuwako na miti miwili iliyosimama katikati yake. Mmoja ulikuwa ni Mti wa Uzima, huo mwingine ulikuwa ni Mti wa Kujua Mema na Mabaya. Mwanadamu alipaswa kuishi kwa Mti wa Uzima; bali hakupaswa kugusa mti huo mwingine la sivyo angekufa. Lakini mwanadamu alikula mti huo mwingine, na wakati alipofanya jambo hilo, mauti ilimwingia kwa njia ya dhambi, naye akatenganishwa na Mungu.

Sasa huo mti kule nyuma katika Edeni, Mti ule ambao ulikuwa ndio chanzo cha uzima, ulikuwa ni Yesu. Katika Yohana, sura ya sita hadi ya nane, Yesu anajiweka Mwenyewe kama chanzo cha uzima wa milele. Yeye alijiita Mwenyewe Mkate kutoka mbinguni. Alinena juu ya kujitoa Mwenyewe na ya kwamba mtu akimla Yeye hatakufa kamwe. Alitangaza ya kwamba alimjua Ibrahimu, na ya kwamba Ibrahimu asijakuwepo, Yeye ALIKUWEKO. Alitabiri ya kwamba Yeye Mwenyewe angewapa maji yaliyo hai ambayo mtu akiyanywa hangeona kiu tena, bali angeishi milele. Alijionyesha Mwenyewe kama MIMI NIKO NILIYE MKUU. Yeye ni Chakula Cha Uzima, Kisima Cha Uzima, Aliye wa Milele, MTI WA UZIMA. Yeye alikuweko kule nyuma katika Edeni katikati ya bustani kama tu vile atakavyokuwa katikati ya bustani ya Mungu.

Wengine wana wazo ya kwamba ile miti miwili katika bustani ilikuwa tu ni miti mingine miwili kama ile mingine ambayo Mungu alikuwa ameiweka mle. Lakini wanafunzi makini wanajua ya kwamba sivyo ilivyo. Wakati Yohana Mbatizaji alipopaza sauti ya kwamba shoka limewekwa kwenye shina la miti yote, yeye hakuwa tu anazungumzia juu ya miti ya kawaida, lakini juu ya kanuni za kiroho. Sasa katika I Yohana 5:11 inasema,

> *"Na huu ndio USHUHUDA, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe."*

Yesu alisema katika Yohana 5:40,

> *"Wala hamtaki kuja Kwangu mpate kuwa na uzima."*

Kwa hiyo ushuhuda, Neno la Mungu, linasema dhahiri na kwa wazi ya kwamba UZIMA, UZIMA WA MILELE, umo katika Mwana. Hauko mahali pengine po pote. I Yohana 5:12,

> *"Yeye aliye Naye Mwana anao huo UZIMA; asiye naye Mwana wa Mungu HANA huo Uzima."*

Sasa, kwa kuwa ushuhuda huo hauwezi kubadilika, kupunguzwa wala kuongezewa, basi huo ushuhuda unasimama ya kwamba UZIMA HUO UMO KATIKA MWANA... Kwa kuwa jambo hili ni kweli, ULE MTI KATIKA BUSTANI HAUNA BUDI KUWA NI YESU.

Sawa. Kama Mti wa Uzima ni mtu, basi Mti wa Kujua mema na mabaya ni mtu PIA. Haiwezi kuwa vinginevyo. Hivyo ndivyo Mwenye Haki na yule Mwovu walivyosimama pamoja pale katikati ya Bustani ya Edeni. Ezekieli 28:13a

> *"Ulikuwa (Shetani) ndani ya Edeni, bustani ya MUNGU."*

Hapa ndipo tunapopokea ufunuo wa kweli wa uzao wa Nyoka. Hivi ndivyo ilivyotukia hasa katika Bustani ya Edeni. Neno linasema ya kwamba Hawa alidanganywa na yule nyoka. Yeye kweli alidanganywa na yule nyoka. Inasema katika Mwanzo 3:1,

> *"Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu."*

Mnyama huyu alikuwa anafanana sana na mwanadamu (na hata hivyo alikuwa mnyama halisi) hata angeweza kuhojiana na kunena. Alikuwa mnyama anayeweza kusimama wima na kwa namna fulani alikuwa kati ya sokwe mtu na mwanadamu, lakini anafanana zaidi na mwanadamu. Alikuwa anafanana sana na mwanadamu hivi kwamba mbegu yake ingeweza, na iliweza kuungana na ya mwanamke na kumfanya abebe mimba. Wakati jambo hili lilipotukia, Mungu alimlaani nyoka. Aligeuza kila mfupa katika mwili wa nyoka hivi kwamba ilimbidi kutambaa kama nyoka. Sayansi inaweza kujaribu iwezavyo, wala haitapata pengo lililopotea. Mungu alihakikisha hatalipata. Mwanadamu ana akili na anaweza kuona uhusiano wa mwanadamu na mnyama na anajaribu kuthibitisha jambo hilo kwa ivolusheni. Hakuna ivolusheni yo yote. Lakini mwanadamu na mnyama walichangamana. Hiyo ni moja ya siri za Mungu ambazo zilibaki zimefichwa, lakini hapa zimefunuliwa. Jambo hilo lilitukia moja kwa moja kule nyuma

katikati ya Edeni wakati Hawa alipoacha Uzima akakubali Mauti.

Angalia yale Mungu aliyowaambia kule bustanini. Mwanzo 3:15,

*"Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na Uzao wake, na Huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino."*

Kama tukikubaliana na Neno ya kwamba mwanamke kweli alikuwa na Uzao, basi nyoka naye bila shaka alikuwa na mzao. Kama Uzao wa mwanamke ulikuwa mtoto mwanamume asiyetokana na mwanamume, basi uzao wa nyoka utapaswa kuwa katika mtindo ule ule, na hiyo ni kusema mwanamume mwingine hana budi kuzaliwa mbali na njia ya mwanamume. Hakuna mwanafunzi asiyejua ya kwamba Uzao wa mwanamke alikuwa ni Kristo aliyekuja kwa njia ya Mungu, mbali na kujuana kimwili kwa binadamu. Inajulikana vizuri pia ya kwamba kule kupondwa kwa kichwa kwa nyoka kulikobashiriwa kwa kweli kulikuwa ni unabii kuhusu yale ambayo Kristo angetimiza dhidi ya Shetani msalabani. Pale msalabani Kristo angekiponda kichwa cha Shetani, naye Shetani angekiponda kisigino cha Bwana.

Sehemu hii ya Maandiko ni ufunuo wa jinsi ambavyo uzao halisi wa nyoka ulivyopandwa duniani, yaani kama vile tulivyo na taarifa ya Luka 1:26-35, ambapo imeandikwa taarifa halisi ya vile Uzao wa mwanamke ulivyodhihirishwa kimwili mbali na njia ya mwanamume.

*"Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti,*

*Kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Mariamu.*

*Na huyo malaika akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu, uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe: umebarikiwa kati ya wanawake.*

*Naye alipomwona, akafadhaika sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani?*

*Malaika akamwambia, Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu.*

*Tazama, utachukua mimba na kuzaa Mtoto Mwanamume; na jina lake utamwita YESU.*

*Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba Yake.*

*Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme Wake utakuwa hauna mwisho.*

*Mariamu akamwambia malaika, Litakuwaje neno hili, maana sijui mume?*

*Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu Zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo Hicho Kitakachozaliwa kitaitwa Kitakatifu, Mwana wa Mungu."*

Kama vile Mzao wa mwanamke ulivyokuwa ni Mungu Mwenyewe kabisa akijizaa katika mwili wa mwanadamu, vivyo hivyo na uzao wa nyoka ni njia halisi ambayo Shetani aliona aliweza kujifungulia mlango wa kuingia katika jamii ya binadamu. Haingewezekana kwa Shetani (kwa maana ni kiumbe cha kiroho KILICHOUMBWA tu) kujizaa katika njia ambayo Mungu alijizaa, kwa hiyo taarifa ya Kitabu cha Mwanzo inasimulia ambavyo yeye alitoa mbegu yake na kuanzisha ama kujiingiza mwenyewe katika jamii ya binadamu. Pia kumbukeni ya kwamba Shetani anaitwa nyoka. Ni uzao wake au kuingizwa kwake katika jamii ya binadamu tunayonena habari zake.

Kabla ya Adamu kumjua Hawa kimwili, nyoka alitangulia kumjua. Na huyo aliyezaliwa kwake alikuwa Kaini. Kaini alikuwa wa (alizaliwa na, alitokana na) "Yule Mwovu." I Yohana 3:12. Roho Mtakatifu ndani ya Yohana hangeweza mahali fulani amwite Adamu "Yule Mwovu" (kwa maana hivyo ndivyo ambavyo angekuwa kama yeye ndiye aliyemzaa Kaini) na katika mahali pengine amwite Adamu "Mwana wa Mungu" ambavyo ndivyo alivyokuwa kwa kuumbwa. Luka 3:38. Kaini aligeuka akawa na tabia kama ya baba yake, anayeleta kifo, mwuaji. Kumkaidi kwake Mungu kabisa wakati alipokabiliwa na Mwenyezi katika Mwa. 4:5,9,13,14, kunamwonyesha yakini kuwa asiye na tabia kabisa ya binadamu, hata alionekana kama amezidi taarifa yo yote tuliyo nayo katika Maandiko ya kuhusu Shetani kukabiliana na Mungu.

*"Bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana.*

*Bwana akamwambia Kaini, Yuko wapi Habili ndugu yako? Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?*

*Kaini akamwambia Bwana, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki.*

*Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso Wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani; hata itakuwa kila anionaye ataniua.*"

Angalia jinsi kumbukumbu ya Mungu inavyoandika taarifa halisi ya kuzaliwa kwa Kaini, Habili na Sethi. Mwanzo 4:1,

*"Adamu akamjua Hawa mkewe, naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana. Akaongezea akamzaa ndugu yake, Habili."*

Mwanzo 4:25,

*"Adamu akamjua mke wake tena; akamzaa mwana mwanamume, akamwita jina lake Sethi..."*

Kuna wana WATATU waliozaliwa kutokana na vitendo VIWILI vya kujuana kimwili kwa Adamu. Kwa kuwa Biblia ni Neno halisi na kamilifu la Mungu, hili si kosa bali ni kumbukumbu la kutuangazia. Kwa kuwa wana WATATU walizaliwa kwa matendo MAWILI ya Adamu, unajua KWA KWELI ya kwamba MMOJA wa hao watatu HAKUWA mwana wa Adamu. Mungu aliandika kumbukumbu hili katika njia hii sahihi kutuonyesha jambo fulani. Ukweli wa mambo ni kwamba Hawa alikuwa na wana WAWILI tumboni mwake (mapacha) kutokana na kuchukua mimba zilizotungwa MBALIMBALI. Yeye alikuwa anabeba mapacha, huku ana mimba ya Kaini ikitangulia kwa kipindi cha muda fulani ile ya Habili. Waone wale MAPACHA tena. Mfano mkamilifu kama ilIvyo sikuzote. Kwa wale wanaofikiria kwamba jambo hili haliwezekani, na ijulikane ya kwamba kumbukumbu za hospitali zimejaa visa ambapo wanawake wamebeba mapacha waliokuwa wa mayai tofauti na wa mimba tofauti zilizobebwa na huku kupata mimba kwa mayai kukiwa kumeachana kwa siku kadha, na ISITOSHE, lakini baadhi ya kumbukumbu hizo zinaonyesha ya kwamba mapacha hao walikuwa wa baba mbalimbali. Hivi karibuni taarifa ilitolewa ulimwengu mzima juu ya mama mmoja wa Kinoruwei aliyekuwa anamshtaki mumewe apate kumtunza yeye na mapacha wake, pacha mmoja akiwa mzungu na huyo mwingine mweusi. Alikubali kwamba alikuwa na mpenzi wa Kinegro. Mimba hizo mbili ziliachana kwa muda wa kama majuma matatu. Katika Beaumont, Texas, mwaka wa 1963, kumbukumbu tena zinaonyesha kuzaliwa kwa watoto kadha ambapo mimba zilikuwa zimeachana kwa siku nyingi, kwa kweli ilikuwa hivi kwamba mwanamke huyo nusura afe na mtoto mmoja katika kuzaa.

Sasa kwa nini jambo hili likatendeka hivyo? Kwa nini ikawa kwamba uzao wa nyoka hauna budi kuja namna hii? Mwanadamu aliumbwa kwa ajili ya Mungu. Mwanadamu alipaswa kuwa hekalu la Mungu. Mahali pa Mungu pa kustarehe (Roho Mtakatifu) palikuwa ni mwanadamu, lile hekalu. Matendo 7:46-51,

*"Aliyepata fadhili mbele za Mungu, naye aliomba ampatie Mungu wa Yakobo maskani.*

*Lakini Sulemani alimjengea nyumba.*

*Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, kama vile asemavyo nabii,*

*Mbingu ni kiti Changu cha enzi, na nchi ni pa kuwekea miguu Yangu: ni nyumba gani mtakayonijengea? asema Bwana, Au ni mahali gani nitakapostarehe?*

*Si mkono Wangu uliofanya haya yote?*

*Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo.*"

Shetani amejua jambo hili tangu zamani. Yeye pia anataka kukaa ndani ya mtu kama vile Mungu anavyofanya. Lakini Mungu amejiwekea Mwenyewe haki hiyo. Shetani hawezi kufanya hivyo. Mungu pekee alitokea katika mwili wa kibinadamu. Shetani asingeweza na hawezi kufanya hivyo. Yeye hana nguvu za kuumba. Njia pekee ya Shetani kutimiza aliyotaka kufanya ilikuwa ni kumwingia yule nyoka kule Edeni yaani kama vile alivyoingia kwa njia ya pepo wachafu katika wale nguruwe Gadara. Mungu hawaingii wanyama; bali Shetani anaweza na atawaingia kutimiliza matakwa yake. Yeye hangeweza kumpata mtoto moja kwa moja kwa Hawa kama Mungu alivyofanya kwa Mariamu, kwa hiyo alimwingia nyoka na akamdanganya Hawa. Yeye alimtongoza na kwa kumtumia Shetani akapata mtoto kwake ili achukue mahali pake. Kaini alikuwa na tabia kamili za kiroho za Shetani na tabia za kinyama (za kimwili, za kimwili) za nyoka. Si ajabu Roho Mtakatifu alisema ya kwamba Kaini alikuwa ni wa yule mwovu. Alikuwa hivyo.

Sasa nataka kuingilia thibitisho fulani tulilo nalo kwamba kuna uhusiano halisi kati ya mwanadamu na mnyama. Ni jambo la kimaumbile. Je! unajua ya kwamba unaweza kuchukua chembechembe hai za mimba kutoka katika kijusu cha mtoto kabla ya kuzaliwa na kuziingiza kwa binadamu? Ndipo hizo chembechembe za kikoromeo zitaingia moja kwa moja mpaka kwenye kikoromeo cha mwanadamu, chembechembe za figo zitaingia moja kwa moja kwenye figo za mwanadamu. Unatambua jinsi jambo hili lilivyo la ajabu sana? Akili fulani huongoza chembechembe hizo za mnyama moja kwa moja kwenye mahali panapopaswa. Akili hiyo

huzikubali chembechembe hizo na kuziweka sawasawa mahali papaswapo. Kuna uhusiano kati ya mnyama na mwanadamu. Hawawezi kuchangamana na kuzaa. Hilo limejaribiwa. Lakini kule nyuma katika ile bustani kuchangamana huko kulitukia na uhusiano wa kemikali uliopo bado unathibitisha jambo hilo. Kwa maana kule nyuma katika Edeni nyoka alikuwa mnyama anayesimama wima. Alikuwa karibu na mwanadamu. Alikuwa karibu ni mtu. Shetani alipata nafasi ya kutumia tabia za maumbile ya yule nyoka apate kumdanganya Hawa. Ndipo Mungu akaangamiza umbile hilo la nyoka. Hakuna mnyama mwingine anayeweza kuchanganyikana na mwanadamu. Lakini uhusiano upo.

Sasa kwa kuwa tumefikia umbali huu, hebu nijaribu kuangazia akili zenu juu ya somo hili ili mweze kuona umuhimu wa sisi kuingilia 'fundiso la uzao wa nyoka' kama nilivyofanya. Tunaanza na kweli kwamba kulikuwa na miti MIWILI katikati ya ile bustani. Mti wa Uzima ulikuwa ni Yesu. Mti ule mwingine hakika ni Shetani kwa sababu ya yale yaliyotokana na tunda la mti huo. Sasa basi, tunajua ya kwamba miti hiyo miwili ilikuwa na uhusiano na mwanadamu la sivyo haingewekwa pale kamwe. Hapana shaka ilikuwa na sehemu katika mpango mkuu na kusudi la Mungu katika uhusiano wao na jamii ya mwanadamu na kwa Yeye Mwenyewe la sivyo hatungeweza kumhesabia Mungu kwamba anajua mambo yote. Hii yote ni kweli kufikia umbali huu, sivyo? Sasa Neno bila shaka linasema ya kwamba kabla ya kuwekwa misingi ya dunia kusudi la Mungu lilikuwa ni kushiriki Uzima Wake wa Milele na mwanadamu. Waefeso 1:4-11,

> *"Kama vile alivyotuchagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele Zake katika pendo.*
>
> *Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake,*
>
> *Na usifiwe utukufu wa neema Yake, ambayo ametuneemesha katika huyo mpendwa.*
>
> *Katika Yeye Huyo, kwa damu Yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake.*
>
> *Naye alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi;*
>
> *Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi Yake, sawasawa na uradhi Wake, alioukusudia katika Yeye Mwenyewe:*
>
> *Kwamba katika madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia; Naam, katika Yeye Huyo:*
>
> *Na ndani Yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi Lake Yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi Yake."*

Ufunuo 13:8,

> *"Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu (Shetani), kila ambaye jina lake halikuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia."*

*Lakini uhai huo haungeweza, wala usingeweza, kugawanywa kwa njia nyingine yo yote mbali na njia ya "Mungu aliyedhihirishwa katika mwili."* Hii ilikuwa ni sehemu ya kusudi Lake la milele na lililokusudiwa tangu zamani. Kusudi hili lilikuwa liwe kwa sifa za utukufu wa neema Yake. Ilikuwa ni mpango wa Ukombozi. Ulikuwa ni mpango wa Wokovu. Sasa sikilizeni kwa makini. "Kwa kuwa Mungu alikuwa Mwokozi, ilikuwa sharti amchague mtu tangu zamani ambaye angehitaji wokovu kusudi ajipe Mwenyewe sababu na kusudi la kuweko." Hilo ni sahihi asilimia mia moja na Maandiko mengi sana yanashuhudia jambo hilo kama vile isemavyo ile aya dhahiri ya Rum. 11:36,

> *"Kwa kuwa VITU VYOTE vyatoka Kwake, viko kwa uweza Wake, tena vinarejea Kwake. UTUKUFU una Yeye milele na milele. Amina."*

Mwanadamu hangekuja moja kwa moja na kushiriki huo Mti wa Uzima ulio katikati ya bustani. Huo Uzima wa Milele wa Mti huo ulipaswa kufanyika mwili kwanza. Lakini kabla Mungu hajaweza kumwinua na kumwokoa mwenye dhambi, Yeye ilibidi awe na mwenye dhambi wa kuinua na kuokoa. Ilibidi mwanadamu aanguke. Huko kuanguka ambako kungesababishwa na Shetani, ilipaswa kupata mwili ili kuwepo na anguko. Ilibidi Shetani apitie katika mwili pia. Lakini Shetani hangeweza kupitia katika mwili wa mwanadamu kusababisha kule kuanguka kama vile ambavyo Kristo angekuja katika mwili wa mwanadamu kuwarudisha walioanguka. Lakini kulikuwako na mnyama, yule nyoka, aliyefanana sana na mwanadamu hata Shetani angeweza kuingia katika mnyama huyo na kwa kupitia mnyama huyo yeye angeweza kuupata mwili wa mwanadamu na asababishe kule kuanguka, na kujiingiza mwenyewe basi katika jamii ya binadamu, kama vile ambavyo Yesu angekuja siku moja na kujiingiza Mwenyewe katika jamii ya binadamu, katika miili ya wanadamu, hata kufikia kwenye ule ufufuo ambapo tutakuwa na miili kama Wake uliotukuzwa. Kwa hiyo yale Mungu aliyotenda hapa bustanini yalikuwa ni mpango Wake uliokusudiwa

tangu zamani. Na wakati Shetani aliposababisha yale yaliyokuwa muhimu kwa kusudi la Mungu, basi mwanadamu hangeweza kuufikia ule Mti wa Uzima pale bustanini. Hakika asingeweza kabisa. Wakati haukuwa umefika. Lakini mnyama (mnyama ndiye aliyekuwa amesababisha kule kuanguka, sivyo? damu ya mnyama na imwagwe) alichukuliwa na damu yake ikamwagwa ndipo Mungu akawa na ushirika na mwanadamu tena. Ndipo kungekuja siku ambayo Mungu angeonekana katika mwili, na kwa njia ya kuaibishwa Kwake Yeye angemrudisha mwanadamu aliyeanguka na kumfanya mshiriki wa Uzima huo wa Milele. Mara unapoona jambo hili, unaweza kufahamu uzao wa nyoka na ujue ya kwamba Hawa hakula tofaa. La, ilikuwa ni kushuka kwa jamii ya wanadamu kwa kuchanganya mbegu.

Sasa najua katika kujibu swali moja lingine halina budi kuzuka, na watu huniuliza, "Kama Hawa alianguka namna hiyo, Adamu alifanya nini, kwa maana Mungu anamlaumu Adamu?" Hilo ni rahisi. Neno la Mungu limedumu milele mbinguni. Kabla ya chembe moja ya vumbi la nyota kuumbwa, Neno hilo (sheria ya Mungu) lilikuwepo VILE VILE KAMA LILIVYOANDIKWA KATIKA BIBLIA YETU. Sasa Neno linatufundisha ya kwamba kama mwanamke akimwacha mumewe na anaenda na mwanamume mwingine yeye ni mzinzi na hana ndoa tena na mumewe hapaswi kumchukua tena. Neno hilo lilikuwa kweli huko Edeni kama lilivyokuwa kweli wakati Musa alipoliandika katika torati. Neno haliwezi kubadilika. Adamu alimrudisha. Yeye alijua vema kabisa kile alichokuwa anafanya, lakini akalifanya jambo hilo hata hivyo. Yeye alikuwa ni sehemu yake, naye alikuwa yuko tayari kuchukua jukumu la Hawa juu yake. Asingemwacha aende zake. Kwa hiyo Hawa akapata mimba yake. Yeye alijua angepata mimba. Alijua kile hasa kingeipata jamii ya binadamu, naye akaiuza jamii ya binadamu dhambini kusudi ampate Hawa, kwa kuwa alimpenda.

Na kwa hiyo hao wana wawili walizaliwa. Wana ambao wangekuwa baba wa jamii ya binadamu ambayo sasa ilikuwa imechafuliwa. Na rekodi inasemaje juu yao? Soma kumbukumbu. Yuda 14,

> *"Na Henoko pia, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii..."*

Mwanzo 5 ni sura ya ukoo wa Henoko. Inaorodhesha ukoo huo hivi,

Adamu, 2. Sethi, 3. Enoshi, 4. Kenani, 5. Mahalaleli, 6. Yaredi, 7. Henoko.

Angalia ya kwamba Kaini hakutajwa. Ukoo wa Adamu unapitia kwa Sethi. Kama Kaini angekuwa ni mtoto wa Adamu, sheria ya mzaliwa wa kwanza ingalimpa Kaini haki katika huo ukoo. Pia haina budi kuangaliwa kwa makini ya kwamba katika Mwanzo 5:3, inasema ya kwamba, "Adamu akaishi miaka mia moja na thelathini, akazaa mwana kwa sura yake, kwa mfano wake, akamwita jina lake Sethi. Hakuna mahali linaposema ya kwamba Kaini alikuwa na sura ya Adamu, hata hivyo ingembidi kuwa sura ya Adamu kama angekuwa mwanae kwa maana sheria ya kuzaana kama inasisitiza ya kwamba kila kitu kizae kwa jinsi yake. Tena hatuna budi kuheshimu ukweli kwamba katika ukuoo ulio katika Mwanzo na pia Luka, Kaini anakosekana. Kama Kaini angalikuwa mwana wa Adamu ingesemwa juu yake mahali fulani ya kwamba, "Kaini, ambaye alikuwa mwana wa Adamu, ambaye alikuwa mwana wa Mungu." Haisemi hivyo kwa kuwa HAIWEZI kusema hivyo.

Naam wanafunzi kwa muda mrefu wameelezea koo mbili za binadamu: mmoja ambao ulikuwa ukoo unaomcha Mungu uonekanao kwa Sethi na huo mwingine ni ukoo usiomcha Mungu kama ulioanzishwa na Kaini. Na ni jambo la ajabu, bali ni kweli, wanafunzi wawa hawa hawajatwambia bado jinsi ilivyokuwa kwamba Kaini alikuwa mtu wa aina ile aliyokuwa wakati Habili na Sethi walikuwa wa ukoo wa kiroho na unaomcha Mungu. Kwa kweli, Kaini angalipaswa kuwa wa kiroho, na Habili asimzidi, na Sethi awe aliyepungukiwa hata na zaidi, na kuendelea kupungua moja kwa moja kwa sababu kila kizazi kinachofuata daima kimeenda mbali zaidi na Mungu. Lakini la, Kaini anatokea akiwa mwovu kuliko mtu ye yote alivyowahi kuelezewa kwa kuwa anashindana vikali na Mungu pamoja na Neno.

Sasa hebu jambo hili na lijulikane: Maandiko hayachezi na maneno. Cho chote kilicho katika Kumbukumbu kiko hapo kusudi macho yenye upako yakione. Iko pale kwa kusudi fulani. Katika Neno hilo inasema, Mwanzo 3:20,

> *"Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa; kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai."*

Lakini hakuna Andiko linalosema ya kwamba Adamu ni baba yao wote walio hai. Kama maana hii haitawekwa juu ya Mwa. 3:20, kwa nini basi itajwe ya kwamba Hawa ndiye mama yao wote, wala hakuna neno lililosemwa juu ya Adamu? Ukweli ni kwamba, ingawa Hawa alikuwa ndiye mama yao wote walio hai, Adamu hakuwa baba yao wote walio hai.

Katika Mwanzo 4:1, Hawa alisema, "Nimepata mtu kwa Bwana." Yeye hamtambui Adamu kuwa baba wa Kaini. Lakini katika Mwanzo 4:25, yeye anasema,

> *"...Maana alisema, Mungu ameniwekea uzao MWINGINE, MAHALI PA HABILI; kwa sababu Kaini alimwua."*

Yeye hasemi ya kwamba Mungu alikuwa AMEMPA uzao mwingine_huo ungekuwa ni Kristo, kwa maana

Yeye ANATOLEWA. Huyu mwana, Sethi, aliteuliwa badala ya Habili. Yeye anamtambua mwanawe aliyetokana na Adamu; yeye hamtambui Kaini kwa kuwa alitokana na yule nyoka. Wakati yeye anaposema UZAO MWINGINE badala ya Habili, anasema ya kwamba Kaini alikuwa tofauti na Habili, kwa maana kama wangalikuwa wa baba yule yule angalipaswa kusema, "Nimepewa UZAO ZAIDI."

Siamini kila ninachosoma, lakini bila shaka ni jambo la ajabu ya kwamba toleo la tarehe 1 mwezi wa Marchi, 1963, la gazeti la LIFE, linaripoti madaktari wa ubongo wakisema jambo lile lile kabisa tunalozungumzia. Sasa najua ya kwamba madaktari wa ubongo wote hawakubaliani wao kwa wao, lakini hivi ndivyo ilivyo. Woga wa nyoka si chukizo litokanalo na kuona bali huja bila ya kuwazia. Kama ingalikuwa hofu ya kawaida watu wangalisimama wakivutiwa vizuri mbele ya matundu ya gorila ama simba. Fahamu zao za bila kuwazia huwafanya waendelee kuwakodolea nyoka macho. Huko kuvutiwa na nyoka ni kwa kujuana kimwili bila mtu kufahamu. Kwamba jambo hilo limekuwa namna hiyo katika nyakati zote inaonekana kwa watu wakipitia katika kizazi baada ya kizazi katika jambo lilo hilo. Nyoka daima wamekuwa na wataendelea kuwa wanaovutia huku wakichukiza. Nyoka daima amesimama kwa mema na mabaya. Amekuwa sanamu ya uume katika nyakati zote. Kama tu vile yalivyo maelezo ya Bustani ya Edeni, tunaona nyoka akiwa mfano halisi wa ashiki.

Karibu imekubalika kabisa kati ya makabila mengi ya kishenzi ya kwamba nyoka anahusishwa na kujuana kimwili na mara nyingi anaabudiwa kuhusiana na jambo hilo. Somo la elimu ya kujuana kimwili linaeleza jambo hilo katika mifano mingi. Sasa ningetaka kujua mahali ambapo watu hawa walipata jambo hilo, kwa kuwa wao hawana elimu wala hawakusoma Biblia kamwe. Lakini kama vile hadithi ya gharika inavyojulikana kila mahali ulimwenguni, vivyo hivyo na kweli hii ya kuanguka kwa mwanadamu ndivyo inavyojulikana. Walijua kilichotukia kule Edeni.

Sasa papa hapa mtu fulani ataniuliza swali hili. Je! Mungu alimwambia Hawa ajihadhari na nyoka la sivyo nyoka angemtongoza? Sasa sikiliza, haikumbidi Mungu kusema cho chote cha yale ambayo yangetokea. Pata tu maana ya hadithi. Yeye alitoa tu Neno. Alisema wasishiriki MAARIFA. Washiriki UZIMA. UZIMA ULIKUWA NI NENO LA MUNGU. MAUTI ILIKUWA NI CHO CHOTE AMBACHO HAKIKUWA NENO LA MUNGU. Yeye aliruhusu NENO MOJA libadilishwe na papo hapo Shetani akamnasa. Mungu angalisema, "Usichume matunda mengi zaidi toka kwenye miti kuliko yale unayoweza kula." Shetani angeweza kusema, "Angalia, hiyo ni kweli kabisa. Mnaona kama ukichuma mengi kupita kiasi yataoza. Lakini hapa pana njia ya kuyahifadhi matunda na hata hivyo wakati huo huo unaweza kuchuma yote utakayo. Kwa hiyo mnaona, unaweza kufanya upendavyo na apendavyo Mungu wakati ule ule." Ibilisi angalimnasa papo hapo. Yeye aliye na hatia katika jambo MOJA la sheria amevunja sheria YOTE. Usicheze na hilo Neno. Hilo ndilo lililotukia hasa katika Wakati wa Efeso kabla haujaisha katika 170 B.K.

Na mti huo ulizaa nini? Mti wa Maarifa ulizaa mauti. Kaini alimwua ndugu yake, Habili. Waovu waliwaua wenye haki. Iliweka kielelezo. Kielelezo hicho kitaendelea mpaka kufanywa upya kwa mambo yote kama ilivyonenwa na manabii.

Huu mti wa Maarifa uliwazaa watu werevu; watu wenye kusifiwa. Bali njia zao ni njia za mauti. Watu wa Mungu ni wa kawaida lakini ni wa kiroho, wakiegemea upande wa Mungu na maumbile, wakiilima ardhi kwa utulivu, wakijali ukweli kuliko mali. Uzao wa nyoka umeleta uchumi mkubwa sana, uvumbuzi wa ajabu, lakini pamoja na hayo yote huja kifo. Baruti zao na bomu za atomiki huua katika vita; na katika wakati wa amani uvumbuzi wao wa mitambo, kama vile motokaa, zitaua hata na zaidi katika wakati wa amani kuliko vile uvumbuzi wa vita unavyoangamiza katika nyakati za shida. Kifo na maangamizi ndiyo mataunda ya kazi yake.

Lakini wao ni wa kidini. Wanamwamini Mungu. Wao ni kama baba yao, ibilisi, na babu yao, Kaini. Wote wawili walimwamini Mungu. Wanaenda kanisani. Wanachanganyikana na wenye haki kama vile magugu yanavyochanganyikana na ngano. Kwa kufanya hivyo wanaharibu na kuzaa dini ya Wanikolai. Wao wanasambaza sumu yao katika kila jitihada ya kuuangamiza uzao wa Mungu kama tu vile Kaini alivyomwua Habili. Hakuna kumcha Mungu mbele ya macho yao.

Lakini Mungu hapotezi ye yote aliye Wake. Yeye huwahifadhi hata katika mauti, Naye ameahidi ya kwamba katika siku ya mwisho Yeye atawafufua.

**NENO LA MWISHO**

*"...Yeye ashindaye, nitampa kula Matunda Ya Mti Wa Uzima, Ulio katika bustani ya Mungu."*

Ni wazo la kusisimua jinsi gani hili. Huo Mti wa Uzima katika Bustani ya Edeni Ambao usingeweza kukaribiwa kwa sababu ya kuanguka kwa Adamu sasa umepewa yeye ashindaye. Ule upanga wa moto wa kerubi alindaye. Lakini haukutiwa alani kabla ubaba wake kujaa damu ya Mwana-Kondoo. Hebu na tutafakari juu ya kweli hii kwa muda kidogo tunapofikiria ni kwa nini Adamu na ukoo wake walikatazwa mti huo lakini sasa umeruhusiwa tena.

Kusudi la Mungu kwa ajili ya kiumbe Chake, mwanadamu, ni kudhihirisha Maneno Yake. Katika

Mwanzo, Adamu alipewa Neno apate kuishi kwalo. Maisha yaliyoishiwa kwa Neno yangekuwa ni Neno lililodhihirishwa. Hiyo ni kweli sivyo? Lakini Adamu aliishi kwa Neno hilo? La, kwa sababu alikuwa aishi kwa KILA Neno, naye alishindwa kutilia maanani kila Neno. Ndipo Musa akatokea. Jinsi alivyokuwa mtu mkuu na mwenye nguvu. Hata hivyo naye pia alishindwa kuishi kwa kila Neno, na nabii huyo, mfano wa yule Nabii Mkuu atakayekuja, alishindwa kwa hasira kulitii Neno. Na kulikuwako na Daudi pia, yule mfalme mkuu wa Israeli, mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu. Alishindwa kwa uzinzi, wakati alipojaribiwa. Lakini hatimaye, katika utimilifu wa wakati, kukaja Mmoja, aliye Kichwa, yaani Yesu, Ambaye pia hana budi kujaribiwa kuona kama ataishi kwa KILA Neno lililotoka katika kinywa cha Mungu. Ndipo Shetani akashindwa. Kwa maana hapa alikuwepo Mmoja Ambaye aliishi kwa "Imeandikwa," na hicho Kipeo cha Mungu kilishinda kwa kuakisi Neno la Mungu. Ndipo huyu Mkamilifu aliyedhihirishwa akapelekwa msalabani, kama Mwana-Kondoo Mkamilifu wa Mungu kwa ajili ya dhabihu kamilifu. Na juu ya ule mti 'Yeye alipata majeraha ya mauti, ili kwamba sisi, kwa njia ya Yeye na kwa sababu Yake, tupate kula ule Mti wa Uzima, na ndipo huo Uzima huo uliotolewa bure ungetuwezesha kushinda, na kulidhihirisha Neno la Mungu.

Na sasa kwa hawa Wana wa Mungu, ambao kwa njia ya Yeye wanashinda, wanapewa haki ya paradiso ya Mungu, na ushirika wa daima wa Yesu Kristo. Hakutakuwako tena na utengano wo wote Naye. Popote aendako, bibi-arusi Wake ataenda. Kile kilicho Chake, Yeye hushiriki na wapenzi Wake katika uhusiano wa mrithi pamoja Naye. Mambo ya siri yatafunuliwa. Mambo ya giza yatadhihirishwa. Tutajua kama tunavyojulikana. Nasi tutakuwa kama Yeye. Huu ndio urithi wa mshindi ambaye ameshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na Neno la ushuhuda kwa Yesu Kristo.

Jinsi tunavyotamani siku hiyo wakati barabara zilizopotoka zote zitanyoshwa, nasi tutakuwa pamoja Naye, wakati usio na mwisho. Jalia siku hiyo na ije upesi, nasi na tuharakishe kulitii Neno Lake na kwa hivyo kuthibitisha kustahili kwetu kushiriki utukufu Wake.

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."* Ni jambo la kusikitisha jinsi gani kwamba wakati huu wa kwanza haukumsikiliza Roho. Badala yake ulimsikiliza mwanadamu. Lakini Mungu na ashukuriwe, katika wakati wa mwisho kutakuwa na kundi fulani litakaloinuka, Bibi-arusi wa Kweli wa siku ya mwisho, naye atamsikiliza Roho. Katika siku hiyo ya giza kuu nuru itarudi kwa Neno safi nasi tutarudi kwenye nguvu za Pentekoste kumkaribisha Bwana Yesu Kristo.

MESSAGE online hub

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7